**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA

KUMB. Na. SO/MC/J.10/4/II/47 TAREHE 01/07/2024

**TANGAZO KWA WANANCHI WOTE WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA.**

**YAH: NIA YA KUTUNGA SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA.**

1. HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA INAWATANGAZIA WANANCHI KUWA INAKUSUDIA KUTUNGA SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI KWA MUJIBU WA KIFUNGU CHA 89 CHA SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI), SURA YA 288 NA KIFUNGU CHA 6 CHA SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA, SURA YA 290.
2. KWA KUZINGATIA MATAKWA YA KIFUNGU CHA 90 (1) CHA SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI), SURA YA 288, KINACHOHUSU JAMII KUTOA MAONI KUHUSU MAPENDEKEZO YA SHERIA ZINAZOTUNGWA NA HALMASHAURI.
3. HIVYO, TUNAWASILISHA MAPENDEKEZO YA SHERIA NDOGO HIZI ILI WANANCHI WAWEZE KUSOMA NA KUTOA MAONI YAO JUU YA SHERIA HIZI.
4. MTU YEYOTE MWENYE MAONI, USHAURI AU PINGAMIZI JUU YA MAPENDEKEZO YA SHERIA HIZI AWASILISHE KWA MAANDISHI NDANI YA SIKU 14 KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI KWA MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA CHUMBA NAMBA 26 (KITENGO CHA HUDUMA ZA SHERIA) AU OFISI YA KATA ILIYO KARIBU.

5. NAKALA ZA RASIMU ZA SHERIA NDOGO HIZI ZINAPATIKANA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA CHUMBA NAMBA 26, OFISI ZOTE ZA MAAFISA WATENDAJI WA KATA PAMOJA NA TOVUTI YA HALMASHURI **www.songeamc.go.tz**.

6. **MAPENDEKEZO YA SHERIA NDOGO HIZI NI KAMA ZIFUATAZO;**

1. SHERIA NDOGO ZA **(USHURU WA MAZAO YA KILIMO NA MISITU)** ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2024.
2. SHERIA NDOGO ZA **(UANZISHAJI NA USIMAMIZI WA MAENEO YA BIASHARA)** ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2024.
3. SHERIA NDOGO ZA **(CHAKULA CHA MCHANA SHULENI)** ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2024.
4. SHERIA NDOGO ZA **(ADA NA USHURU**) ZA HALAMSHAURI YA MANISPAA ZA MWAKA, 2024.
5. SHERIA NDOGO ZA **(KUDHIBITI UCHINJAJI HOLELA WA MIFUGO)** ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2024.
6. SHERIA NDOGO ZA **(UPULIZIAJI VIUATILIFU**) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2024.
7. SHERIA NDOGO ZA (**USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI**) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2024.
8. SHERIA NDOGO ZA **(KUDHIBITI UBORA WA VYAKULA NA MAJENGO YA VYAKULA)** ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2024.
9. SHERIA NDOGO ZA **(KUDHIBITI UTILILISHAJI WA MAJITAKA)** ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2024.
10. SHERIA NDOGO ZA **USAFI WA MAZINGIRA (MAREKEBISHO)** ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2024.

……………………………………

Wakili Bashir P. Muhoja

MKURUGENZI WA HALMASHAURI

MANISPAA SONGEA

**Tangazo la Serikali Na. ___________ La Tarehe _____________**

**SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA**

**(SURA YA 290)**

**SHERIA NDOGO.**

**Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16 (1)**

**SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO YA MISITU NA KILIMO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA, 2024.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jina la Sheria Ndogo** | **1.** | | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao ya Misitu na Kilimo) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka, 2024 |
| **Matumizi** | **2.** | | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote yaliyo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea na zitaanza kutumika kuanzia tarehe ya kutangazwa katika gazeti la Serikali. |
| **Tafsiri** | **3.** | | Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:- |
| | | | **Afisa Mwidhiniwa’’** ni Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi<br><br>**“Halmashauri”** Maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Songea.<br><br>**“Mazao ya Kilimo’’** Maana yake ni mazao yatokanayo na rasilimali zitokanazo na kilimo kama vile mahindi, maharage, soya, ufuta, alizeti nk.<br><br>‘’**Mazao ya misitu’’** Maanayake ni mazao yatokanayo na rasilimali ya misitu kama vile mkaa, mbao, kuni, asali, mianzi nk.<br><br>“**Mkurugenzi’’** maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea au Afisa yeyote aliyekaimishwa ofisi hiyo akitekeleza majukumu ya Mkurugenzi.<br><br>**“Ushuru”** maana yake ni malipo yanayolipwa kwa halmashauri kutokana na mazao ya misitu na kilimo. |
| **Utozaji wa ushuru** | **4.** | (1) | Halmashauri inaanzisha utaratibu wa kutozaushuru wa mazao ya misitu na kilimo, kwa mazao yote ya misitu na kilimo na la pili |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | yanayozalishwa katika halmashauri na yanayoingia katika halmashauri bila kutozwa ushuru katika maeneo yalikozalishwa kwa Mujibu wa jedwali la kwanza na jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi. |
| | | (2) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kila msafirishaji wa mazao ya misitu na kilimo ndani ya halmashauri anatakiwa kuhakikisha analipia ushuru wa mazao yake anayosafirisha kulingana na viwango vilivyobainishwa na Halmashauri. |
| | | (3) | Malipo yote ya ushuru yatafanyika kwa njia ya fedha taslimu kupitia kwa wakala au mkusanya ushuru wa halmashauri na kisha kupewa stakabadhi ya kieletroniki ya kuthibitisha malipo hayo (EFD). |
| | | (4) | Mkurugenzi anayo mamlaka kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kuamuru uzuiaji wa mazao ya misitu na kilimo yanayosafirishwa bila kulipiwa ushuru unaotozwa na halmashauri, |
| **Ukusanyaji wa ushuru wa mazao ya kilimo** | **5** | (1) | Ili kurahisisha ukusanyaji wa ushuru wa mazao ya kilimo, halmashauri inaweza kukusanya ushuru huo kwa mfumo wa shilingi baada ya kufanya mahesabu kutokana na viwango vya asilimia vilivyobainishwa katika jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi. |
| | | (2) | Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kifungu cha 5 (1) hapo juu, Halmashauri italazimika kufanya mapitio ya viwango vya ushuru wa mazao ya kilimo kila mwisho wa mwaka wa fedha ili kuendana au kukaribiana na bei ya soko ya mazao ya kilimo kwa kipindi kinachofuata cha mwaka mpya wa fedha. |
| | | (3) | Ili mapitio mapya ya viwango vya ushuru wa mazao ya kilimo yaanze kutumika sharti yapate kibali cha kamati ya utawala na fedha ya halmashauri na muhtasari kwa kikao husika utasomwa pamoja na Sheria Ndogo hizi na utakuwa sehemu ya Sheria Ndogo hizi. |
| **Wajibu wa msafirishaji wa mazao ya misitu na kilimo** | **6** | | Kila Msafirishaji wa mazao ya misitu na kilimo ndani ya halmashauri atakuwa na wajibu wa kuzingatia yafuatayo;<br><br>a. Analipia ushuru wa mazao ya misitu na kilimo anayosafirisha bila shuruti,<br>b. Anapokea stakabadhi ya kieletroniki kutoka kwa mkusanya ushuru wa halmashauriau wakala baada ya malipo, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | c. Anatunza nyaraka zote muhimu zinazohusiana na mzigo anaosafirisha.<br>d. Anapata kibali kutoka halmashauri cha kusafirisha mazao ya kilimo nje ya manispaa kwa mujibu wa jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi. |
| **Uanzishaji wa Vituo vya ukaguzi** | **7** | | Ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi, Halmashauri inaanzisha vituo mbalimbali vya ukaguzi wa mazao ya misitu na kilimo yanayosafirishwa nje ya halmashauri kwa mujibu wa jedwali la nnela Sheria Ndogo hizi. |
| **Mamlaka ya kufanya ukaguzi vituoni.** | **8** | | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, halmashauri inayo mamlaka ya kisheria kufanya ukaguzi wa mazao ya misitu na kilimo yanayosafirishwa ili kujiridhisha juu utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi. |
| | **9** | | Litakuwa ni jukumu la kisheria kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kwa mtu yeyote anayesafirisha mazao ya misitu na kilimo ndani ya halmashauri kuhakikisha anafuata na kuheshimu matakwa ya sheria Ndogo hizi. |
| **Uteuzi wa wakala** | **10** | (1) | Halmashauri inaweza kumteua wakala wa kukusanya ushuru wa mazao ya misitu na kilimo katika eneo lote au sehemu ya eneo la mamlaka ya halmashauri. |
| **1Wajibu wa wakala** | **11** | | Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa;<br>a. Kukusanya na kupokea ushuru kutoka kwa kila mtu anayetakiwa kulipa ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.<br>b. Kuwasilisha benki kila siku fedha alizokusanya kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi au mkataba wa uwakala.<br>c. Kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi ikiwemo vibarua wake. |
| **Makosa ya wakala** | **12** | (1) | Wakala yeyote atakuwa ametenda makosa kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo atafanya moja wapo kati ya makosa yafuatayo;<br>a. Atashindwa kuwasilisha benki kiasi chote cha fedha ya ushuru alichokusanya,<br>b. Atatoza kiwango cha ushuru kwa mfanyabiashara kinyume na viwango vilivyoainishwa na sheria Ndogo hizi,<br>c. Atatoa taarifa za uongo kwa njia yoyote kuhusu idadi ya waliolipa au |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | wanaostahili kulipa ushuru au suala lolote linalohusiana na kazi yake ya uwakala chini ya mkataba wake na halmashauri<br>d. Atashindwa kutekeleza majukumu yake ya uwakala ipasavyo,<br>e. Atakusanya ushuru katika maeneo ambayo hayakuainishwa katika mkataba wake wa uwakala,<br>f. Atatorosha wafanyabiashara kwa lengo la kukwepa kulipa ushuru. |
| | | (2) | Wakala yeyote atakayekiuka Sheria Ndogo hizi atachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa adhabu zinazotolewa na Sheria Ndogo hizi. |
| **Wajibu wa Afisa muidhiniwa** | **13.** | (1) | Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuzuia na kushikilia mazao ya misitu na kilimo yanayosafirishwa bila kulipiwa ushuru baada ya kuamuriwa kufanya hivyo na Mkurugenzi. |
| | | (2) | Endapo mazao ya misitu na kilimo yaliyokamatwa na kushikiliwa kwa kushindwa kulipiwa ushuru yatashindwa kulipiwa ushuru ndani ya kipindi cha siku saba (7) kuanzia tarehe ya kukamatwa, Afisa muidhiniwa atatoa tangazo la siku saba (7) kwa umma la nia ya kuuza mazao hayo, baada ya siku saba za tangazo kuisha halmashauri itauza mazao hayo kwa mnada, isipokuwa mazao yanayoharibika ndani ya muda mfupi tangazo litatolewa ndani ya muda wa masaa sita (6) tu. |
| | | (3) | Endapo Halmashauri itatumia gharama yoyote katika kutekeleza mamlaka yake chini ya Sheria Ndogo ya 13 (2) gharama hizo zitarejeshwa mara moja na mtu aliyesababisha hasara hiyo. |
| | | (4) | Kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi, halmashauri haitawajibika kwa hasara zozote zitakazotokana na kukamata, kuzuia na kuuza mazao ya misitu na kilimo yanayosafirishwa kinyume na masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi. |
| **Muda wa kusafirisha mazao ya misituna kilimo** | **14** | | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Mazao ya misitu na kilimo yatasafirishwa kwa muda wote wa masaa ishirini na nne ya siku, isipokuwa mazao ya misitu yamayotokana na miti pori yatasafirishwa kuanzia saa12.00 asubuhi na mwisho utakuwa saa 12.30 jioni |
| **Makosa na adhabu** | **15** | (1) | Mtu yeyote ambaye;<br>(a) Atasafirisha mazao ya misitu na kilimo bila kulipia ushuru, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | (b) Atamzuia Afisa muidhiniwa kutekeleza majukumu yake,<br>(c) Atamshawishi mtu mwingine asilipe ushuru,<br>(d) Atatorosha mazao ya misitu na kilimo kwa lengo la kukwepa kulipa ushuru,<br>(e) Atatoa takwimu za uongo juu ya mazao ya misitu na kilimo anayoyasafirisha kwa lengo la kukwepa kulipa ushuru sahihi,<br>(f) Atakataa kusimama katika vituo vya kukagulia mazao ya misitu na kilimo,<br>(g) Atatoa lugha ya kashfa au kejeli kwa Afisa muidhiniwa katika utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br>(h) Atakataa kulipia ushuru wa mazao ya misitu na kilimo,<br>(i) Atasafirisha mazao ya misitu yatokanayo na miti pori kabla ya saa 12.00 asubuhi na baada ya 12.30 jioni. |
| | | (2) | Mtu huyo atakuwa amekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi, na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi za kitanzania milioni moja 1,000,000/= au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote kwa pamoja kifungo na faini. |
| **Kufifilisha kosa** | **16** | | Iwapo mtu aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi atakiri makosa kabla ya shauri halikufikishwa mahakamani na kulipa faini kwa hiari, Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa lake baada ya mkosaji kujaza fomu ya kukiri kosa hilo kwa mujibu wa Jedwali la tano la Sheria Ndogo hizi. |

**JEDWALI LA KWANZA**

**USHURU WA MAZAO YA MISITU**
**(Chini ya kifungu cha 4 (1))**

| NA. | AINA YA ZAO | KIASICHAADA /USHURU. |
|---|---|---|
| 1 | Mkaa Mti wa porini | Tshs.1,000/= kwa gunia la kilo 50. |
| 2 | Mkaa mti wa kupandwa | Tshs.5,000/= kwa guniia la kilo 50 |
| 3 | Mbao laini (Miti ya kupandwa) | Tshs.300/= kwa kila ubao. |
| 4 | Mbao ngumu (Mti pori) daraja la kwanza | Tshs.14,575/= kwa mita ya ujazo 1 |
| 5 | Mbao ngumu (Mtipori) daraja la pili | TShs.13,000/= kwa mita ya ujazo 1 |
| 6 | Mbao ngumu (Mti pori) daraja la tatu | Tshs.9,750/= kwa mita ya ujazo 1 |
| 7 | Kuni za miti ya kupandwa | Tshs.2,000/= kwa mita ya ujazo 1 |
| 8 | Kuni miti ya porini | Tshs.325/= kwa mita ya ujazo 1 |
| 9 | Nguzo za miti ya kupanda<br>Nguzo za Umeme | Tshs. 300/= kwa nguzo 1<br>10,000/= kwa nguzo 1 |
| 10 | Mabanzi | Tshs.100/= kwa kila banzi moja |
| 11 | Ada ya kusajili biashara ya mazao ya misitu na viwanda vya kuchakata na kutengeneza bidhaa zitokanazo na mazao ya Misitu | 5% ya gharama ya ada ya usajili wa wizara |
| 12 | Ada kukata mti wa kupandwa | Tshs.10,000/= kwa mti mmoja wenye ukubwa wa Zaidi ya kipenyo cha sentimita 30. |
| 13 | Kitanda mti wa kupandwa | Tshs.6,000/= kwa kitanda1 |
| 14 | Kitanda Mtipori | Tshs.4,000/= kwa kitanda1 |
| 15 | Fremu za milango na madirisha mti wa kupandwa | TSHS.4,000/= kwa fremu 1 |
| 16 | Fremu za milango na madirisha mti pori | Tshs.2,590/= kwa fremu 1 |
| 17 | Vifuniko ya milango mti wa kupandwa | Tshs.6,000/= kwa mlango 1 |
| 18 | Vifuniko vya milango mti pori | Tshs.2,525/= kwa mlango 1 |
| 19 | Kabati la mti wa kupandwa | Tshs.6,000/= kwa kabati 1 |

| | | |
|---|---|---|
| 20 | Kabatila mti pori | Tshs.2,500/= kwa kabati 1 |
| 21 | Kiti/stuli ya mti wa kupandwa | Tshs.2,000/= kwa kiti/ stuli 1 |
| 22 | Kiti/stuli ya mti pori | Tshs.9,000/= kwa kiti/stuli 1 |
| 23 | Dawati la shule la mti pori | Tshs.900/= kwa dawati 1 |
| 24 | Meza ya chakula mti wa kupandwa (Office table) | Tshs,6,000/= kwa meza 1 |
| 25 | Meza ya chakula mti pori (Office table) | Tshs.1,500/= kwa meza i |
| 26 | Kochi la seti moja mti pori | Tshs.1,500/= kwa seti m1 |
| 27 | Kochi la moja mti wa kupandwa | Tshs 6,000/ kwa seti 1<br><br>Tshs. 2000/= kwa kila kochi linaongezeka baada ya seti |
| 28 | Vikapu | Tshs.500/= kwa kilo1 |
| 29 | Samani zingine ndogo (Other wooden small items) | Tshs.500/= kwa kila samani |
| 30 | Asali | Tshs. 500/= kwa lita 1 |
| 31 | Mtumbwi wa mti wa kupandwa | Tshs.10,000/=kwa mtumbwi 1 |
| 32 | Mtumbwi wa mti pori | 5% ya ushuru uliotozwa na wizara kwa kila mtumbwi 1 |
| 33 | Vinyago | 5% ya ushuru uliotozwa na wizara kwa kila kg1 |
| 34 | Mikeka | Tshs. 500/= kwa kila mkeka |
| 35 | Fagio | Tshs.200/= kwa kila mfagio |
| 36 | Vinu vikubwa | Tshs.1000/= kwa kila kinu |
| 37 | Vinu vidogo | Tshs. 500/= kwa kila kinu |
| 38 | Nyungo | Tshs. 200/=kwa kila ungo |
| 39 | Magamba/Mizizi ya Miti | Tshs. 500/= kwa kilo 1 |
| 40 | Mianzi | Tshs’ 2000/= kwa mianzi 10 |
| 41 | Kufanya Picnic/utalii kwenye Msitu wa hifadhi wa Halmashauri | Tshs. 3000/= kwa kila mtu kwa siku<br><br>Tshs.10,000/= kwa gari dogo kwa siku. |

| | | |
|---|---|---|
| 42 | Kufanya utafiti katika Msitu wa Hifadhi wa Halmashauri | Tshs. 20,000/= kwa Siku 1 |
| 43 | Ada ya kuweka mnara wa mawasiliano katika msitu wa hifadhi wa Halmashauri | Tshs. 300,000/= kwa mwezi kwa eneo la ukubwa wa urefu wa mita 15 na upana wamita 15 |
| 44 | Ada ya kuchukua udongo, mchanga au kifusi katika katika msitu wa hifadhi wa Halmashauri | Tshs. 12,000/= kwa kila tani 1 |

**JEDWALI LA PILI**

**USHURU WA MAZAO YA KILIMO**

**(Chini ya kifungu cha 4 (1))**

| NA. | AINA YA ZAO | KIASICHA USHURU. |
|---|---|---|
| 1 | Soya | 3% ya bei ya mauzo ya soko, kwa gunia la kg 100 |
| 2 | Mbaazi | 3% ya bei ya Mauzo ya soko, kwa gunia la kg 100 |
| 3 | Viazi vitamu | 3% ya bei ya mauzo ya soko, kwa gunia la kg 100 |
| 4 | Viazi Mviringo | 3% ya bei ya mauzo ya soko, kwa gunia la kg 100 |
| 5 | Vitunguu maji | 3% ya bei ya mauzo ya soko, kwa gunia la kg 100 |
| 6 | Vitunguu Swaumu | 3% ya bei ya mauzo ya soko, kwa gunia la kg100 |
| 7 | Maharage | 3% ya bei ya mauzo ya soko, kwa gunia la kg 100 |
| 8 | Mahindi | 3% ya bei ya mauzo ya soko, kwagunia la kg 100 |
| 9 | Mpunga/Mchele | 3% ya bei ya mauzo ya soko, kwa gunia la kg 100 |
| 10 | Ngano | 3% ya bei ya mauzo ya soko,kwa gunia la kg 100 |
| 11 | Choroko | 3% ya bei ya mauzo ya soko, kwagunia la kg 100 |
| 12 | Mtama | 3% ya bei ya mauzo ya soko,kwa gunia la kg 100 |
| 13 | Ulezi | 3% ya bei ya mauzo ya soko,kwa gunia la kg 100 |
| 14 | Dengu | 3% ya bei ya mauzo ya soko,kwa gunia la kg 100 |
| 15 | Karanga | 3% ya bei ya mauzo ya soko,kwa gunia la kg 100 |
| 16 | Mihogo | 3% ya bei ya mauzo ya soko,kwa gunia la kg 100 |
| 17 | Pumba | 3% ya bei ya mauzo ya soko,kwa gunia la kg 100 |
| 18 | Alizeti | 3% ya bei ya mauzo ya soko, kwa gunia la kg 100 |
| 19 | Kahawa | 3% ya bei ya mauzo ya soko, kwa gunia la kg 100 |
| 20 | Ufuta | 3% ya bei ya mauzo ya soko, kwa gunia la kg 100 |
| 21 | Mtama | 3% ya bei ya mauzo ya sok, kwa gunia la kg 100 |
| 22 | Kunde | 3% ya bei ya mauzo ya soko, kwa gunia la kg 100 |
| 23 | Machungwa | 1000/= kwa gunia moja<br>5000/= kwa gari ya tani moja<br>15,000/= kwa gari ya tanimbili<br>30,000/= kwa gari tani 3 hadi 5 |
| 24 | Matikiti maji | 1000/= kwa gunia moja<br>5000/= kwa gari ya tani moja<br>15,000/= kwa gani ya tani mbili |

| | | |
|---|---|---|
| | | 30,000/= kwa gari ya tani 3 hadi 5 |
| 25 | Maembe | 1000/= kwa tenga moja<br>1000/= kwa gunia moja |
| 26 | Ndizi | 500/= kwa mkungu 1<br>1000/= kwa tenga 1 |
| 27 | Nyanya | 500/= kwa tenga dogo<br>1000/= kwa tenga kubwa |
| 28 | Kabichi | 1000/= kwa gunia 1 |
| 29 | Pumba | 500/= kwa gunia 1 la kg 100 |
| 30 | Mashudu | 500/= kwa gunia moja la kg 100 |
| 31 | Karoti | 1000/= kwa gunia la kg 100 |
| 32 | Nazi | 1000/= kwa gunia la kg 100 |
| 33 | Matunda mengine | 1000/= kwa gunia moja<br>5000/= kwa gari ya tani moja<br>15,000/= kwa gani ya tani mbili<br>30,000/= kwa gari ya tani 3 hadi 5 |

JEDWALI LA TATU

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

[NEMBO YA HALMASHAURI]

HATI NA. ……………………….. Tarehe ……………………...

**KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAZAO YA KILIMO NJE YA HALMASHAURI**

*(Chini ya Sheria Ndogo 6 (d))*

(Ijazwe na Msafirishaji)

1. Jina la Msafirishaji ………………………………………..Namba ya simu…………………
2. Jina La Kampuni/ Shirika/ …………………………………
3. Anuani yake S. L. P. ………… Simu: …………………………. Wilaya ………………
4. Mahali ofisi yake ilipo; Mtaa ……..……. Kata ……………….. Wilaya …………………
5. Namba ya leseni ya biashara ……………………………………………
6. Eneo ambalo mzigo unatoka ……………………………………………………….
7. Jina la zao linalosafirishwa…………………………………………………..
8. Kiasi cha mzigo kinachosafirishwa……………………………………….
9. Kiasi cha ushuru wa Mazao kinachostahili kulipwa Halmashauri na Msafirishaji kulingana na mzigo anao safirishwa………………………………………
10. Eneo ambalo mzigo unaenda ……………………………………………..

**NATHIBITISHA** Kuwa maelezo yote niliyotoa hapo juu ni sahihi na kweli.

Jina la Msafirishaji …………………………………………………………………

Saini ya Msafirishaji……………………………………………………………...

Tarehe ……………………………………………………………………………….

**SEHEMU YA CHINI IJAZWE NA AFISA MTENDAJI KATA UNAKOTO MZIGO.**

Muda wa kibali hiki ni kuanzia tarehe …………………. Mpaka tarehe ………………………..baada ya muda huu kuisha kibali hiki kitakuwa batili.

Nakala ya kibali itunzwe na msafirishaji kwa ajili ya ukaguzi wakati wowote:

Nakala ya kibali hiki itabaki kwa:

Afisa Mtendaji wa kata.

__________________________________

Afisa Mtendaji wa Kata

**JEDWALI LA NNE**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**
**(NEMBO YA HALMASHAURI)**
**VITUO VYA UKAGUZI WA USHURU WA MAZAO YA MISITU NA KILIMO**
**(Chini ya kifungu cha 7).**

| NA | JINA LA KITUO | JINA LA KATA |
|---|---|---|
| 1 | Lilambo | LILAMBO |
| 2 | Mletele | MLETELE |
| 3 | Chandarua ‘A’ | MSHANGANO |
| 4 | Chandarua “B” | MSHANGANO |
| | Shule ya Tanga | TANGA |
| 6 | Chemchem | MATOGORO |
| 7 | Gawaza | MATOGORO |
| 8 | Subira | SUBIRA |
| 9 | Londoni | LIZABONI |
| 10 | Mwengemshindo | MWENGEMSHINDO |

**JEDWALI LA TANO**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

**(NEMBO YA HALMASHAURI)**

**HATI YA KUKIRI KUTENDA KOSA**

**(Chini ya Kifungu 16)**

Mimi …………………………………………… Nakiri mbele ya Bw/Bi ………………………… Mkurugenziwa Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwambaMnamo tarehe...................... Ya Mwezi …………….. mwaka ……………nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu namba …………………………….. Cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao ya Misitu na Kilimo) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka, 2024.

Nipo tayari kulipa kiasi cha faini kinachodaiwa ambacho ni Tshs. ________________________ badala ya kupelekwa Mahakamani, ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 16 cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu huku nikifahamu kuwa nilichofanya ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao ya Misitu na kilimo) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka 2024

Jina la Mkosaji:________________________________________Saini__________________________

Alama ya dole gumba _______________________________Tarehe _______________saa________

**Mbele ya Ushahidi wa.**

Jina:________________________________________________Saini___________________________

Alama ya dole gumba _________________________________

Tarehe_________________________

Maelezo ya Mkurugenzi ______________________________________________________________

Jina laMkurugenzi: ________________________________________

Saini ya Mkurugenzi: _______________________________________

Tarehe ____________________________

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea iligongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutanowa Baraza la Madiwani wa Halmashauri yaManispaa ya Songea uliofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri tarehe …………. Mwezi …………,2024 na Lakiri hii iligongwa mbele ya:

________________________________

BASHIR P. MUHOJA.
**MKURUGENZI HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA.**

________________________________

MICHAEL LEODGAR MBANO
**MSTAHIKI MEYA HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA.**

NAKUBALI

________________________________

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS,**
**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)**

**DODOMA**
TAREHE _________

**SHERIA YA SERIKALI ZAMITAA (MAMLAKA ZA MIJI)**

**SURA YA 288/2002.**

**SHERIA NDOGO.**

**Zimetungwa chini ya kifungu cha 89.**

**SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI NA USIMAMIZI WA MAENEO YA BIASHARA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2024.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jina la tarehe ya kuanza kutumika** | **1.** | | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Uanzishaji na Usimamizi wa Maeneo ya Biashara) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka, 2024 na zitaanza kutumika mara baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali. |
| **Eneo la kutumika** | **2.** | | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea. |
| **Tafsiri** | **3.** | | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:- |
| | | | **"Afisa Muidhiniwa"** Maana yake Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>**"Halmashauri"** Maana yake Halmashauri ya Manispaa ya songea.<br><br>'**Maeneo ya biashara**' maana yake ni maeneo maalum yaliyotengwa rasmi na halmashauri kwa ajili ya aina mbalimbali za biashara.<br><br>**"Mkurugenzi"** Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea na ni pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.<br><br>**'Mtaa"** maanayake ni mtaa ulioanzishwa kwa Mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Sura ya 288) ambako maeneo yaliyotengwa na yasiyoruhusiwa kwa biashara yapo<br><br>**"Wakala"** Ina maana ya mtu binafsi, kikundi cha watu, Kampuni, Taasisi, Shirika au Serikali ya Mtaa atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi' |
| **Uanzishaji wa maeneo ya biashara** | **4.** | (1) | Halmashauri imeanzisha maeneo maalumu kwa ajili ya kufanya biashara ndani ya halmashauri kwa mujibu wa jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi. |
| | | (2) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kila Mfanyabiashara ambaye hana eneo rasmi la kufanya biashara analazimika kufanya biashara katika maeneo yaliyotengwa na Halmashauri kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | (3) | Mfanyabiashara anayekusudia kufanya biashara katika maeneo yaliyoanzishwa na halmashauri atalazimika kuwasilisha maombi ya nafasi kwa kujaza fomu kwa Mujibu wa Jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi. |
| | | (4) | Mfanyabiashara mdogo aliyeko kwenye eneo rasmi atatakiwa kulipa ushuru kama atatumia meza/ kizimba au kodi ya pango kwa yule anayetumia kibanda cha tofali au mbao kwa mujibu wa Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka, 2024. |
| **Maeneo yasiyo rasmi** | 5 | (1) | Kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi, maeneo yasiyo rasmi ni pamoja na vichochoro vya mitaa, kandokando ya barabara, mbele ya maduka, nje ya majengo ya serikali na ya watu binafsi na n je ya masoko. |
| **Katazo kwa mfanyabiashar** | 6 | (1) | Mfanyabiashara yoyote hataruhusiwa kufanya yafuatayo;<br>a. Kuendesha biashara yake nje soko au eneo lolote lisilo rasmi,<br>b. Kufanya biashara pembezoni mwa barabara,<br>c. Kufanya biashara katika eneo lililo rasmi bila kuwa na mkataba na halmashauri<br>d. Kuendesha biashara bila kulipa ushuru / kodi,<br>e. Kugawa eneo alilokabidhiwa na halmashauri au kupangisha eneo hilo kwa mtu mwingine,<br>f. Kumiliki meza /vizimba katika maeneo ya halmashauri kwa lengo la kufanya biashara ya kupangisha. |
| **Wajibu wa mfanyabiashara** | **7** | (1) | Utakuwa ni wajibu wa kila Mfanyabiashara ndani ya halmashauri kufanya yafuatayo;<br>a. Kuhakikisha anafanya biashara katika maeneo yaliyotengwa rasmi na halmashauri<br>b. Kuepuka kufanya biashara katika maeneo yaliyozuiliwa na halmashauri.<br>c. Kutumia eneo la biashara kulingana na matumizi yaliyopangwa na halmashauri. |
| **Wajibu wa Mtaa** | **8** | | Kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kila Mtaa utakuwa na wajibu ufuatao;<br>a. Kuhakikisha maeneo yaliyotengwa na halmashauri katika kila mtaa yanafanya kazi ipasavyo.<br>b. Kuunda kamati ndogo ya Mtaakwa ajili ya kusimamia ufanyikaji wa biashara katika maeneo yaliyotengwa na halmashauri.<br>c. Kuhakikisha wafanyabiashara hawafanyi biashara katika maeneo yasiyo rasmi katika mtaa husika.<br>d. Kusimamia na kutoa taarifa kwa halmashauri juuya ukiukwaji wa taratibu zilizowekwa na halmashauri na kuchukua hatua za kisheria kwa wakosaji. |
| **Wajibu wa kata** | **9** | | Kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi,kila Kata itakuwa na wajibu ufuatao; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | a. Kushirikianana uongozi wa Mtaa kuhakikisha wafanyabiashara wanafanya biashara katika maeneo yaliyotengwa na Halmashauri yaliyopo katika kata husika.<br>b. Kuhakikisha kamati za mitaa zilizopo katika kata husika zinatekeleza majukumu yake ipasavyo.<br>c. Kuhakikisha hakuna wafanyabiashara wanaofanya biashara katika maeneo yaliyozuiliwa na Halmashauri.<br>d. Kutatua changamoto zinazoibuliwa na mtaa katika suala zima la wafanyabiashara kutakiwa kufanya biashara katika maeneo yaliyotengwa na Halmashauri.<br>e. Kutoa taarifa kwa Halmashauri juu ya changamoto zilizojuu ya uwezo wa kata katika kuzitatua. |
| **Wajibu wa halmashauri** | **10.** | (1) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, halmashauri inao wajibu wa kisheria kuhakikisha imetenga maeneo ya kufanyia biashara ndani Halmashauri na kuhakikisha maeneo yanafanyiwa biashara ili kutimiza azma yake. |
| | | (2) | Halmashauri ina wajibu wa kisheria kuhakikisha huduma zote muhimu katika maeneo ya biashara zinapatikana ili kurahisisha utendaji kazi wa wafanyabiashara katika maeneo yaliyotengwa. |
| **Maeneo ya watu binafsi** | **11.** | (1) | Itakuwa ni kosa kwa mtu au taasisi kuruhusu eneo lake kufanyiwa biashara bila kibali cha Halmashauri kinyume na matakwa ya Mipango Miji na masharti ya mipango miji yaliyotolewa katika umilikiwa eneo hilo. |
| | | (2) | Kwa mujibu wa sheria ndogo hizi, halmashauri inayo mamlaka ya kufunga maeneo yoyote ndani ya halmashauri ambayo yanatumika kufanya biashara bila kupata kibali cha manispaa ikiwepo kuanzisha biashara katika maeneo ambayo hayajaruhusiwa. |
| **Wajibu wa kulipa ada mbalimbali** | **12.** | | Utakuwa ni wajibu kwa kila mfanyabiasharaanayetumia maeneo ya biashara yaliyotengwa rasmi na Halmashauri kuhakikisha anafuata masharti yote yaliyowekwa katika maeneo hayo ikiwepo kulipa ada zote zinazotakiwa kulipwa katika maeneo husika. |
| **Uteuzi wa Wakala /Afisa muidhiniwa** | **13.** | (1) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Halmashauri inaweza kumteua Wakala kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi; |
| | | (2) | Wakala atakayeteuliwa na Halmashauri atakuwa na jukumu la kuhakikisha matakwa ya Sheria Ndogo hizi yanatekelezwa na kutoza faini kwa niaba ya Halmashauri kama ilivyoelezwa na Sheria Ndogo hizi; |
| **ukaguzi wa maeneo** | **14.** | (1) | Halmashauri inaweza kuanzisha timu mbalimbali ndani ya Halmashauri kwa madhumuni ya kukagua ili kujiridhisha |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | juu ya utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi. |
| | | (2) | Ukaguzi utahusisha uhakiki wa maeneo ambayo yamezuiliwa kufanyiwa biashara. |
| | | (3) | Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 14 (1) cha Sheria Ndogo hizi, halmashauri inaowajibu wa kisheria kufanya ukaguzi katika maeneo yote yaliyotengwa kwa biashara ndani ya halmashauri ili kujiridhisha endapo wafanyabiashara wamezingatia matakwa ya Sheria Ndogo hizi. |
| **Makosa na adhabu** | **15.** | (1) | Mtu yeyote ambaye:-<br>a) Atafanya biashara katika maeneo yasiyoruhusiwa,<br>b) Atatumia eneo lake la biashara kufanya biashara isiyokusudiwa na Halmashauri,<br>c) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukiuka matakwa ya Sheria Ndogo hizi,<br>d) Atakataa au kushindwa kutii maagizo ya Afisa Muidhiniwa au Wakala,<br>e) Atajenga au kuweka kibanda cha biashara katika maeneo yasiyotengwa rasmi,<br>f) Atamzuia Afisa Muidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake,<br>g) Atatishia uhai wa wakala au Afisa Muidhiniwa wakati akitekeleza majukumu yake,<br>h) Atalazimisha kufanya biashara katika maeneo yasiyoruhusiwa,<br>i) Atakataa kuhamia kwa hiari katika maeneo yaliyotengwa na Halmashauri kuhusiana na biashara yake,<br>j) Atatangaza hadharani kuwazuia watu wengine wasitekeleze matakwa ya Sheria Ndogo hizi,<br>k) Atafanya biashara barabarani au pembezoni mwa barabara, |
| | | (2) | Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na atashtakiwa mahakamani na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi mia mbili elfu tu ((**Tshs;200,000/=) na isiyozidi shilingi 1,000,000/= ( milioni moja)** au kifungo cha miezi isiyozidi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja; |
| | | (3) | Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kifungu cha 15 (2) cha Sheria Ndogo hizHalmashauri inaweza kutaifisha mali zilizokamatwa katika maeneo yasiyoruhusiwa kufanya biasharakwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na kuzigawa kwenye Taasisi zinazohusiana na malezi ya watu wenye mahitaji au wagonjwa katika hospitali mbalimbali kulingana na aina ya bidhaa iliyokamatwa. |
| | | (4) | Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuuza kwa mnada mali za wafanyabiashara zilizokamatwa kwa mujibu wa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | masharti ya kifungu cha 15(3) cha Sheria Ndogo hizi, endapo mfanyabiashara atashindwa kulipa faini kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi. |
| | | (5) | Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea kwa mtu yeyote ambaye bidhaa zake zimekamatwa na kupigwa mnada, kwa kutekeleza mamlaka yake kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi. |
| **Kufifilisha kosa** | **16.** | | Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote yule endapo mkosaji, atakiri kosa lake kwa maandishi kwa kujaza hati ya Kukiri ktenda kosa kwa Mujibu wa Jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini. |

**JEDWALI 'LA KWANZA**

**MAENEO YA BIASHARAZA MASOKO, STENDI NA VITUO VYA MABASI YALIYOTENGWA**
**(Chini ya kifungu cha 4(1).**

| Na. | ENEO LILILOTENGWA | AINA YA BIASHARA ILIYORUHUSIWA |
|---|---|---|
| (i) | Soko la Bombambili | Matunda, Viazi na Vitunguu kwa jumla |
| (iii) | soko la Mfaranyaki | Dagaa na Samaki |
| (iv) | Soko la mazao Msamala | Nafaka za aina zote. |
| (v) | Soko la Green Belt | Mitumba ya Viatu na Nguo na bidhaa nyingine mbalimbali za mitumba |
| (vi) | Soko kuu la Manispaa | Bidhaa mchanganyiko |
| (vii) | Soko la Manzese 'a" | Bidhaa mchanganyiko |
| (viii) | soko la Manzese "b" | Bidhaa mchanganyiko |
| (iX) | Soko la Lizaboni | Bidhaa Mchanganyiko |
| (x) | Soko la Mjimwema | Bidhaa mchanganyiko |
| (xi) | Soko la Mshangano | Mbogamboga na Matunda |
| (xii) | Soko la Majengo | Bidhaa Mchanganyiko |
| (xiii) | Stendi kuu ya shule ya Tanga | Kituo Kikuu cha Mabasi ya Mikoani |
| (xiv) | Stendi ya Mfaranyaki | Stendi ya Daladalla |
| (xv) | Kituo cha  Seedfarm | Kituo kidogo cha Mabasi |
| (xvi) | Kituo cha Majengo | Kituo kidogo cha mabasi |
| (xvii) | Kituo cha Ruhuwiko | Kituo kidogo cha Mabasi |
| (xviii) | Soko la jioni barabara ya Litunu | Mbogamboga na Matunda ( Kuanzia 12.00 jioni kila siku) |
| (xix) | Barabara ya Majengo | Bidhaa za Mitumba ( Kuanzia saa 10.00 Jioni kila siku) |

**JEDWALI LA PILI**

**FOMU YA MAOMBI YA KUFANYA BIASHARA**

**(Chini ya kifungu cha 4 (3))**

**SEHEMU 'A'**

**(Ijazwe na Mwombaji)**

Majina ya Mwombaji--------------------------------wa Sanduku la barua----------------Songea.

Kuwasilisha ombi la kufanya biashara ya ________________________________ katika eneo la ---------------------------------------------------------- --------------------------- katika mtaa wa---------- -------------------- kata ya------------------------------------------Manispaa ya Songea.

Nipo tayari kufuata masharti yote yaliyobainishwa katika Sheria Ndogo za (Uanzishaji na Usimamizi wa Maeneo ya Biashara) za Manispaa ya Songea, 2024

Saini ya Mwombaji------------------------------------------------Tarehe-------------------------------

**SEHEMU 'B'**

**(Kwa matumizi ya Ofisi)**

**MAONI YA AFISA MTENDAJI WA MTAA.**

Nashauri Mwombaji aruhusiwe/asiruhusiwe kufanya Biashara;

TOA SABABU________________________________________________________Jina la Afisa Mtendaji__________________________Saini_____________MHURI___________

**MAELEKEZO YA MKUU WA IDARA YA VIWANDA ,BIASHARA N A UWEKEZAJI;**

Mwombaji aruhusiwa/Asiruhusiwe kufanya biashara katika eneo la_________________Mtaa wa________________kata ya ________________

Saini-----------------------------------------Tarehe--------------------------------Mhuri___________

## JEDWALI LA TATU

## HATI YA KUKIRI KWA HIARI KUTENDA KOSA.

**(Chini ya kifungu cha 16).**

Mimi:_________________________nakiri mbele ya Bw/Bi:______________Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwamba mnamo tarehe:_______________ya mwezi_________mwaka___________nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu namba__________________cha Sheria Ndogo za **(Uanzishaji na Usimamizi wa Maeneo ya Biashara**) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea, za mwaka 2024.

Nipo tayari kulipa kiasi cha faini kinachodaiwa ambacho ni Tshs_______________badala ya kupelekwa Mahakamani ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamalaka aliyopewa chini ya kifungu cah 16 cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwahiari yangu kadri ya ufahamu wangu huku ni kifahamu kuwa nilichofanya ni kosa kwa mujibu wa Sheira Ndogo za **(Uanzishaji na Usimamizi wa Maeneo ya Biashara)** za Halmashauri ya Manispaa ya Songea, za mwaka 2024.

Jina la Mkosaji:____saini_______alama ya dole gumba _________tarehe______________

**Mbele ya Shahidi:**

Jina:_______________________________Saini________________________Alama ya dole gumba:__________________________tarehe:______________________________________

Maelezo ya Mkurugenzi kwa kifupi:-
Jina la Mkurugenzi:____________________________________________________________
Saini ya Mkurugenzi:___________________________________________________________
Tarehe:_______________________________________________________________________
Mhuri:________________________________________________________________________

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea iligongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuata azimio laMkutano wa Baraza la Madiwani ulioketi Ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songeatarehe ________________mwezi____________mwaka, 2024, na kushuhudiwa na:-

______________________________________

BASHIR P. MUHOJA,

**MKURUGENZI HALMASHAURI YA MANISPAA**

**SONGEA.**

______________________________________

MICHAEL LEODGAR MBANO

**MSTAHIKI MEYA HALMASHAURI YA MANISPAA**

**SONGEA.**

**NAKUBALI;**

______________________

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (**MB),**

**WAZIRI WA NCHI-OFISI YA RAIS,**

**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA).**

**DODOMA**

**Tarehe:____________________**

Tangazo la Serikali Na ……………. La Tarehe…………..

**SHERIA YA SERIKALI ZAMITAA (MAMLAKA ZA MIJI)**

**SURA YA 288**

**(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 89)**

**SHERIA NDOGO ZA (CHAKULA CHA MCHANA SHULENI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEAZA MWAKA, 2024**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jina** | **1.** | | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (**Chakula cha Mchana Shuleni)** za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka 2024na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. |
| **Matumizi** | **2.** | | Sheria Ndogo hizizitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Manispaa ya Songea. |
| **Tafsiri** | **3.** | | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itahitajika vinginevyo:-<br><br>‘’**Afisa Muidhiniwa’’** maana yake ni Afisa Mtendaji wa Kata au mtaa, pamoja na Mtumishi yeyote atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>**“Bodi ya shule**“maana yake ni Bodi inayosimamia uendeshaji wa shule ya Sekondari Tanzania.<br><br>**“Chakula cha Mchana”**maana yake ni chakula kinachoandaliwa kwa ajili ya kuliwa na watoto wakati wa mchana na inajumuisha chai au uji.<br><br>**“Halmashauri**” Maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Songea.<br><br>**“Kamati ya shule’**maana yake ni kamati ya uendeshaji wa shule za msingi inayoundwa na wazazi/walezi na wataalam.<br><br>**‘Kamati ya chakula”**maana yake ni kamati ndogo katikashule inayosimamia masuala ya chakula.<br><br>“**Mchana”** maana yake ni wakati wote kati ya saa12.30 asubuhi hadi saa12 jioni kila siku ambao mtoto anahudhuria shuleni.<br><br>“**Mkurugenzi**’’ Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.<br><br>**“Mzazi’’** Maana yake ni mzazi wa biolojia wa mtoto, mlezi wa mtoto, au taasisi ambayo inajukumu kwa muda husika la kulea mtoto husika.<br><br>“**Shule”** maana yake ni shule za Msingi au Sekondari za Serikali zilizopo katika Halmashauri. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | **'Shule Mahsusi'** maana yake ni shule ambayo mwanafunzi anasoma na mzazi /mlezi anatakiwa kuchangia chakula.<br><br>**'Taarifa ya uchangiaji'** maana yake ni taarifa inayotolewa katikangazi ya shule kila mwezi kuhusu mapato na matumizi ya michango ya chakula katika shule mahsusi. |
| **Agizo la wanafunzi kula shuleni** | **4.** | (1) | Halmashauri inaanzisha utaratibu wa lazima kwamba kila mtoto anayesoma katika shule yeyote ya Awali,Msingi au Sekondari ya kutwa katika eneo la Halmashauri atakuwa na haki isiyo ya hiari kupata na kula chakula cha mchana shuleni. |
| **Wazazi kuchangia chakula** | **5** | (1) | Itakuwa ni wajibu wa kila mzazi kuchangia chakula kwa ajili ya mwanae au mwanafunzi anayemlea, anayesoma katika shule yoyote ndani ya eneo la Halmashauri kwa kiwango cha michango kama ilivyooneshwa katika jedwali la Sheria hizi. |
| | | (2) | Michango yote ya Wazazi itakusanywa na Kamati za Wazazi zitakazoundwachini ya Sheria Ndogo hizi, na itahifadhiwa katika akaunti maalum ya Wazazi iliyopo au itakayofunguliwa katika Halmashauri husika. |
| | | (3) | Michango yote ya chakula itakayokusanywa na kamati ya wazazi itahifadhiwa na kamati husika katika chumba kilichotengwa na shule na kukabidhiwa kwa kamati ya wazazi kwa ajili ya kuhifadhia vyakula. |
| **Kamati za Wazazi** | **6** | (1) | Kila shule ya Msingi au sekondari ya umma au ya serikali itakuwa na kamati maalum ya Wazazi kwa ajili ya kukusanya,kuratibu,kuhifadhi na kufanya matumizi ya fedha za michango ya chakula katika Shule husika. |
| | | (2) | Kamati ya wazazi itakuwa na wajumbe wasiopungua watatu na wasiozidi watano watakaochaguliwa katika mkutano wa wazazi na walezi wote wenye watoto wanaosoma kwenye shule husika. Jinsi izingatiwe ambapo miongoni mwa wajumbe hao lazima pawepo na mwanamke mmoja (1). |
| | | (3) | Kamati ya Wazazi itadumu madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu, lakini mjumbe anaweza kuchaguliwa tena katika vipindi visivyozidi vitatu. |
| | | (4) | Kazi za kamatizitafanyika kwa Msingi wa kujitolea, isipokuwa wakati wa kufanya kazi za kukusanya michango au kufanya manunuzi ya chakula, gharama za usafiri wa wajumbe zinaweza kutolewa katika fedha za chakula. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi ya fedha na aina za Vyakula** | **7** | (1) | Fedha zitakazochangwa zitatumika kwa ajili ya gharama za posho za wapishi , ununuzi wa viungo na gharama za kusaga mahindi. |
| | | (2) | Katika kupika chakula, kamati husika itawajibika kufuata kanuni za chakula bora na mlo kamili .Kwa madhumuni ya Sheria Ndogo hizi, mlo kamili utakuwa mlo unaojumuisha mboga za majani. |
| | | (3) | Vyakula vitakavyopikwa na kamati vitakuwa vile vinavyopatikana kwa urahisi katika eneo la Halmashauri ambavyo vinaliwa na wanajamii walio wengi. |
| | | (4) | Itakuwa ni marufuku kwa kamati au walimu kuchangisha vyakula ambavyo haviliwi na baadhi ya wanajamii kwa sababu za kiimani kama vile nyama ya Nguruwe,mbwa,panya na wanyama wengine ambao, kulingana na utamaduni wa Watanzania, wanyama hao hawaliwi na wanajamii walio wengi. |
| **Mamlaka ya Kamati** | **8.** | | Kamati itakuwa na mamlaka yafuatayo pamoja na yale yanayoweza kuongezwa kwake kwa azimio maalum la Halmashauri;<br>(a) Kukusanya michango kutoka kwa wazazi,walezi au wahisani au wadau wengine wa maendeleo ndani nanje ya Manispaa.<br>(b) Kwa kushirikiana na idara za Elimu ndani ya Halmashauri, kuamua kuhusu kula au kutokula kwa mtoto yoyote ambaye mzazi au mlezi wake hajachangia chakula.<br>(c) Kuchukua hatuakwa wazazi wasiochangia fedha za chakula shuleni ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kisheria kuwashtaki mahakamani, na inaweza kuchukua hatua hizo kwa kushirikiana au bila kushirikiana na Halmashauri.<br>(d) Kutoa ushauri kwa walimu kuhusu aina ya chakulla kinachopaswa kuliwa na watoto katika shule husika.<br>(e) Kuchukua hatua pale ambapo mpishi au wapishi wanapika chakula chini ya kiwango kinachotarajiwa.<br>(f) Kusoma taarifa ya mapato na matumizi ya michango ya chakula katika Kamati ya shule au Bodi ya shule husika.<br>(g) Kumiliki vitabu maalum vya stakabadhi za kukusanyia michango ya chakula, ni sharti vitabu hivyo viidhinishwe na Halmashauri kabla ya kuanza kutumika. |
| **Mamlaka ya Mkurugenzi** | **9** | (1) | Mkurugenzi au Afisa mwingine aliyeruhusiwa na Mkurugenzi anaweza kuvunja Kamati ya Chakula ya Shule yoyote ikiwa itathibitika kuwa wajumbe wa kamati hiyo wamefanya moja kati ya mambo yafuatayo; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | (a) Wamekusanya na kutumia michango kwa madhumuni mengine mbali na chakula katika shule husika.<br>(b) Wameshindwa kusimamia ukusanyaji wa michango bila sababu za msingi.<br>(c) Wamepoteza uaminifukwa waliowachagua kwa misingi kwamba mienendo ya Wajumbe inakiuka misingi ya uadilifu.<br>(d) Wanajihusisha na masuala ya rushwa na ubadhilifu wa aina yoyote. |
| | | (2) | Katika kuchukua hatua ya kuvunja Kamati husika Mkurugenzi atashauriana na Diwani na Mwenyekiti wa Mtaa ambapo shule husika imo, na baada ya uamuzi huo, atatoa taarifa kwenye kikao cha Kamati ya Huduma za Jamii kilichopo karibu. |
| **Makosa** | **10** | | Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote endapo;<br>(i) Atakaidi au kushindwa kuchangia fedha za Chakula shuleni kwa kiwango kilichoelezwa ndani ya Sheria Ndogo hizi;<br>(ii) Atatamka maneno ya matusi,kuudhi au kashfa dhidi ya mjumbe yeyote wa kamati ya chakula au atamzuia kufanya shughuli zake,<br>(iii)Atamzuia au kujaribu kumzuia mtoto kuhudhuria masomo ili kukwepa kutoa mchango wa chakula.<br>(iv)Atashawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa mchango wa chakula;<br>(v) Atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji, au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa mchango wa chakula au mchango mwingine wowote ndani ya Halmashauri.<br>(vi)Kwa makusudi huku akijua ni kosa, atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au atashindwa kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri.<br>(vii) Ikiwa mjumbe au wajumbe watashindwa kuweka kumbukumbuza vitabu vya hesabu au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri au katika chombo kingine chochote cha serikali au umma chenye mamlaka kisheria;<br>(viii) Atamzuia Afisa Muidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake;<br>(ix)Atakwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi; |
| **Adhabu** | **11** | | Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili **(200,000/=)** na isyozidi shilingi milioni moja **(1,000,000/=)** au kifungo kisichopungua miezi kumi na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne (24) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo,. |
| **Kufifilisha kosa** | **12** | | Mkurugenzi anaweza kumtoza Mtu yeyote faini isiyopungua shilingi Hamsini Elfu (50,000/=) na isiyozidi shilingi laki mbili (200,000/=) iwapo mkosaji kwa hiari yake mwenyewe atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake kwa kulipa mchango husika na kulipa faini |

**JEDWALI LA KWANZA**

**AINA ZA SHULE NA VIWANGO**

**(Chini ya kifungu cha 4)**

| **Na.** | **AINA YA SHULE** | **AINA YA VYAKULA** | **MUDA** |
|---|---|---|---|
| 1. | Awali | a. Mchele kilo 6<br>b. Tshs 10,000/= kwa ajili ya gharama za kununua viungo na malipo ya mpishi. | Kwa Muhula mmoja<br><br>Kwa muhula mmoja |
| 2. | Msingi | a. Mahindi dumla 8<br>b. Maharage dumla 3<br>c. Tshs.15,000/= kwa ajili ya gharama za kusaga,kununua viungo na malipo ya mpishi | Kwa Muhula mmoja<br><br>Kwa muhula mmoja<br><br>Kwa muhula mmoja |
| 3. | Sekondari | a. Mahindi dumla 10<br>b. Maharage dumla 3<br>c. Tshs 20,000/= kwa ajili ya gharama za Kusaga, kununulia viungo na malipo ya mpishi | Kwa muhula mmoja<br><br>Kwa muhula mmoja<br><br>Kwa Muhula mmoja |

## JEDWALI LA PILI

## HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA.

**(Chini ya kifungu cha 12)**

Mimi …………………………………………………….…………wa anuani ………………..… ninayefanya shughuli ya ………………………………………………….. ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea, nakiri kutenda kosa la …………………………………….. ikiwa ni kinyume na kifungu cha sheria ndogo ya (Chakula cha mchana shuleni) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka 2024.

Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe pasipo kushawishiwa na mtu yeyote nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekelezanmadaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 12 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini ………………………………………………………………

Mbele yangu;

Jina ………………………………………………………………….

Saini …………………………………………………………………

Cheo; Mkurugenzi

Lakiri ya Halmashauri yaManispaa ya Songea imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatiaazimio lililopitishwakwenye Mkutano wa Halmashauri ulioitishwa na kufanyika katika Ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea tarehe…………. Mwezi …………,Mwaka 2024 na kubandikwa mbele ya;

____________________________________

BASHIR P. MUHOJA.

**MKURUGENZI HALMASHAURI YA MANISPAA**

**SONGEA.**

____________________________________

MICHAEL LEODGAR MBANO

**MSTAHIKI MEYA HALMASHAURI YA MANISPAA**

**SONGEA.**

NAKUBALI

**………………………………….**

MOHAMED OMARY MCHENGERWA(MB)

**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS,**

**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)**

**DODOMA**

TAREHE …..../………./…….

**Tangazo la Serikali Na. ___________ La Tarehe _____________**

**SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA**

**(SURA YA 290)**

**SHERIA NDOGO.**

**Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16 (1)**

SHERIA NDOGO ZA (**ADA NA USHURU**) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA, 2024.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jina la Sheria Ndogo** | **1.** | | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za ( Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka, 2024 |
| **Matumizi** | **2.** | | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote yaliyo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea na zitaanza kutumika kuanzia tarehe ya kutangazwa katika gazeti la Serikali. |
| **Tafsiri** | **3.** | | Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:- |
| | | | **'Ada na Ushuru'** maana yake ni tozo au malipo yanayolipwa na mtu yeyote kwa halmashauri kwa ajili ya kupata kibali na huduma.<br>**Afisa Mwidhiniwa''** ni Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br>**"Halmashauri"** Maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Songea.<br>'Kibanda" maana yake ni chumba chochote cha biashara kilichojengwa kwa tofali au mbao katika eneo linalomilikiwa na halmashauri.<br>"Kibali cha ujenzi" maana yake ni kibali kinachotolewa na halmashauri kwa mmiliki wa kiwanja au jengo ili aweze kukiendeleza kwa kujenga au kufanya ukarabati.<br>"Kituo cha mabasi" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria.<br>"Kizimba / meza" maana yake ni eneo au kipande cha eneo alichogawiwa mtu na Halmashuari kwa ajili ya kuweka bidhaa zake na kuuza ndani ya masoko ya halmashauri. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | “Kodi ya pango” maana yake ni tozo itakayolipwa na mtu yeyote aliyepanga katika nyumba, jengo, kizimba au kibanda cha biashara kinachomilikiwa na halmashauri pamoja na vibanda vya biashara vilivyojengwa kwa ubia na watu binafsi katika maeneo yanayomilikiwa na halmashauri.<br>“Maegesho” maana yake ni maeneo maalumu yaliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha magari.<br>“Mabango” maana yake ni ubao, maandishi au kitu chochote ambacho kimeandikwa kwa madhumuni ya kutangaza biashara fulani.<br>“**Machinjio”** Maana yake ni eneo maalum lililotengwa na halmashauri au kuruhusiwa na halmashauri kwa ajili ya huduma ya kuchinja wanyama au kuanika ngozi za wanyama waliochinjwa.<br>“Madini ya ujenzi’ maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa, na madini mengine yanayotumika katika ujenzi.<br>“Mfanya biashara” maana yake ni mtu yeyote anayenunua na au kuuza bidhaa mbalimbali ndani ya halmashauri.<br>“Mkoa” maana yake ni Mkoa wa Ruvuma.<br>“**Mkurugenzi”** maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea au Afisa yeyote aliyekaimishwa ofisi hiyo akitekeleza majukumu ya Mkurugenzi.<br>“Mazao ya uvuvi” maana yake ni mazao yote yatokanayo na shughuli za uvuvi, kwa mfano dagaa, Samaki n.k.<br>“Sherehe” maana yake ni harusi, sendoff, kipaimara, komunyo, muziki wa kibiashara, na mashindano mengine yoyote ya ngoma za asili.<br>“Soko” maana yake ni eneo lililotengwa na linalomilikiwa na halmashauri kwa ajili ya huduma za kuuza na kununua bidhaa.<br>“Stakabadhi” maana yake ni hati ya kieletroniki inayotolewa na halmashauri au wakala kwa lengo la kukiri kupokea malipo ya ada au ushuru.<br>“Ushuru wa huduma” maana yake ni ushuru unaotozwa kwa mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara kutokana na mauzo ya biashara yake. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | "Wakala" maana yake ni mtu, taasisi, kikundi cha watu, kampuni au Asasi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi. |
| **Utozaji wa Ada na ushuru** | **4.** | (1) | Halmashauri itatoza ada, ushuru na kodi ya pango katika mazingira mbalimbali kama ilivyoorodheshwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi. |
| | | (2) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, utakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa ushuru, ada au kodi ya pango kufanya hivyo. |
| | | (3) | Mtu yeyote atakayelipa ada, ushuru au kodi ya pango chini ya Sheria Ndogo hizi, atapewa stakabadhi halali ya kieletroniki kuthibitisha malipo hayo (EFD). |
| | | (4) | Mtu yeyote atakayefanya malipo na kupewa stakabadhi halali ya halmashauri atawajibika kuitunza na haitakuwa ni utetezi kudai kuwa stakabadhi aliyopewa imepotea, imeharibika au ameisahau eneo tofauti na eneo linalofanyiwa ukaguzi. |
| | | (5) | Ada na ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi, utalipwa kwa halmashauri au wakala aliyeteuliwa na halmashauri kwa ajili ya kukusanya ada, ushuru au kodi ya pango. |
| **Muda wa kulipa ada,kodi na ushuru** | **5** | (1) | Mtu yeyote anayetakiwa kulipa ada, ushuru au kodi ya pango atalipa kulingana na muda uliotajwa katika Sheria Ndogo hizi au mkataba wake na halmashauri. |
| | | (2) | Mtu yeyote atakayechelewa kulipa ada, ushuru au kodi ya pango kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, atalipa pamoja na faini ya asilimia ishirini kwa muda ambao atakuwa amecheleweshwa malipo. |
| **Wajibu wa Mfanyabiashara** | **6** | (1) | Utakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara katika maeneo ya soko, mnada, vibanda na magulio chini ya Sheria Ndogo hizi, kuhakikisha kwamba analipa ada , ushuru au kodi ya pango kadri ya Sheria Ndogo hizi na mikataba aliyofunga na halmashauri. |
| **Ukusanyaji wa madeni ya ada,ushuru na kodi** | **7** | | Ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi, endapo mtu yeyote anayetakiwa kulipa ada, ushuru au kodi ya pango atakataa au kushindwa kulipa ndani ya muda unaotakiwa, halmashauri inaweza kuchukua hatua za kisheria dhidi yake ikiwemo kutoza faini, kufungiwa biashara na kusitisha huduma. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mamlaka ya Kukamata na kuuza mali** | **8** | (1) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa ana mamlaka ya kufunga, kuzuia au kukamata bidhaa au chombo cha mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ada, ushuru au kodi ya pango ili kushinikiza malipo kwa mujibu wa **jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.** |
| | | (2) | Halmashauri inaweza kuiomba mahakama kutoa amri ya kuuza mali zilizokamatwa au kuzuiwa kwa njia ya mnada pale ambapo mtu anayestahili kulipa ada, ushuru au kodi ya pango amegoma au ameshindwa kulipa. |
| | | (3) | Halmashauri kabla kuomba kibali cha mahakama kuuza mali zilizokatwa, itatoa taarifa ya maandisha ya masaa sita (6.) kwa wahusika kwa bidhaa ambazo zinaharibika haraka, na taarifa ya siku saba (7) kwa bidhaa zisizoharibika haraka ikimtaarifu mmiliki, mtumiaji au mtu yeyote ambaye mali yake inatarajiwa kuuza. |
| | | (4) | Endapo mmiliki wa biashara au huduma ameshindwa kulipa ada, ushuru au kodi ya pango anayodaiwa ndani ya muda uliotolewa katika kifungu cha 8 (3) hapo juu, mazao, bidhaa, chombo au jengo vitauzwa na halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi. |
| | | (5) | Baada ya kuuza mali iliyoshindwa kulipiwa ushuru, Mkurugenzi atawajibika kufanya yafuatayo;<br>a. Kukata ushuru ,ada au kodi ya pango inayodaiwa pamoja na faini ya ucheleweshaji iliyokuwa inadaiwa,<br>b. Kukata gharama zote za mnada , ulinzi na usafiri . |
| | | (6) | Kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi, halmashauri haitawajibika kwa namna yoyote kwa hasara itakayotokana na uharibifu wa mali utakaotokea wakati wa ukusanyaji wa ada, ushuru, kodi ya pango, madeni au kuhifadhi mali zilizokamatwa au kuzuiwa na halmashauri. |
| **Mamlaka ya kuingia** | **9** | | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi, wakala au Afisa mwidhiniwa wanaweza kuingia katika jengo au mahali popote na wakati wowote kwa ajili ya kukagua au kukusanya mapato. |
| **Uteuzi wa** | **10.** | | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi,Halmashauri inaweza |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Wakala** | | | kumteua wakala wa kukusanya ushuru, ada au kodi ya pango katika eneo lote au sehemu ya eneo la halmashauri kwa ajili ya kukusanya madeni,ushuru au ada |
| Wajibu wa wakala | 11 | | Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo hizi , atakuwa na wajibu ufuatao;<br>a. Kukusanya na kupokea ushuru au ada kutoka kwa kila mtu anayetakiwa kulipa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi,<br>b. Kuwasilisha kila siku katika akaunti za halmashauri fedha zote alizokusanya kwa siku husika kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi au mkataba wa uwakala,<br>c. Kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi.<br>d. Kutunza mahesabu/ stakabadhi za malipo yote ya makusanyo yote ya ushuru au ada aliyoyafanya na kuwasilisha halmashauri.<br>e. Kuomba ujira wa kazi yake ya uwakala kwa wakati na kwa maandishi kwa halmashauri. |
| Makosa ya wakala | 12 | (1) | Wakala yeyote atakuwa ametenda kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo;<br>a. Atashindwa kuwasilisha halmashauri kiasi chote cha fedha ya ada au ushuru alichokusanya,<br>b. Atashindwa kuwasilisha fedha alizokusanya katika akaunti za halmashauri kwa kila siku,<br>c. Atatoza kiwango cha ada au ushuru kwa mtu yeyote kinyume na viwango vilivyobainishwa katika Sheria Ndogo hizi,<br>d. Atatoa taarifa za uongo kwa njia yoyote kuhusu idadi ya waliolipa au waliostahili kulipa ada au ushuru au suala lolote linalohusiana na kazi yake ya uwakala chini ya mkataba wake na halmashauri,<br>e. Atashindwa kutekeleza wajibu wake kama wakala chini ya Sheria Ndogo hizi,<br>f. Atakusanya ada au ushuru katika maeneo ambayo hayakuainishwa katika mkataba wake wa uwakala. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | (2) | Wakala yeyote atayekiuka Sheria Ndogo hizi atachukuliwa hatua za kisheria. |
| Kibali cha ujenzi/Ukarabati | **13** | (1) | Itakuwa ni kinyume na Sheria Ndogo hizi, kwa mtu yeyote kujenga , kurekebisha jengo, kukarabati jengo au kuendeleza ardhi bila kulipa ada ya kibali cha ujenzi na kupewa kibali cha ujenzi kutoka halmashauri kwa mujibu wa **jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi** |
| | | (2) | Mtu yeyote anayetaka kufanya shughuli yoyote kati ya shughuli zilizotajwa katika kifungu cha 13(1) hapo juu, atatakiwa kuwasilisha maombi kwa ajili ya kupata idhini akiambatanisha na nyaraka zifuatazo;<br>Kwa jengo la kawaida;<br>a. Ramani ya jengo ikionyesha mpangilio wa jengo (Floor Plan),pande zote za nyumba (Elevation), mchoro unaoonyesha jengo kuanzia msingi hadi kupaua (Section)<br>b. Nakala kivuli ya hati ya kiwanja iliyothibitishwa kisheria/Barua ya toleo (Offer).<br>c. Mkataba wa mauziano ya kiwanja ( kama ipo)<br>d. Stakabadhi ya malipo mengine ya serikali.<br>e. Stakabadhi ya malipo ya ada ya upimaji.<br>f. Nyaraka nyingine zozote zinazohusu kiwanja kinachotaka kujengwa.<br>Kwa jengo la ghorofa au Maghala;<br>a) Ramani iliyochorwa na kugongwa mhuri wa Msanifu majengo anayetambuliwa (Architectural Drawings),<br>b) Ramani iwe yenye michoro ya kihandisi iliyochorwa na kugongwa mhuri na Mhandisi (Structural Drawings),<br>c) Ramani iwe na vipimo ya udongo ( Geotechnical Survey Report),<br>d) Awe na ripoti ya mazingira (EIA). |
| | | (3) | Ni marufuku kwa mtu yeyote katika eneo lote la mamlaka ya halmashauri kujenga jengo, ukuta, sehemu yoyote ya jengo iliyobomoka au kubomolewa kwa makusudi kwa ajili ya ukarabati au marekebisho ya jengo bila kibali cha ujenzi cha halmashauri. |
| | | (4) | Sheria Ndogo hizi, zinatoa katazo kwa mtu yeyote katika maeneo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | yaliyotangazwa kuwa ya mipangomiji, kubadili matumizi ya kiwanja au jengo kutoka matumizi au sura ya jengo kwenda kwenye matumizi / sura nyingine au kwa ajili ya matumizi mengine bila kibali. |
| | | (5) | Maombi ya kibali cha ujenzi yatawasilishwa halmashauri kwa kutumia fomu maalum iliyotolewa kwa mujibu wa **jedwali la nne la Sheria Ndogo hizi**. |
| | | (6) | Endapo ujenzi wowote utakiuka masharti ya yaliyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka na uwezo kisheria kufanya yafuatayo;<br>a. Kumwamuru mmiliki avunje jengo hilo kwa gharama zake mwenyewe ndani ya muda utakaokuwa umeamuriwa katika amri hiyo.<br>b. Kuchukua hatua dhidi ya mmiliki wa eneo husika.<br>c. Kusimamisha ujenzi unaofanyika na kumwamuru mmiliki afanye marekebisho kulingana na masharti ya kibali cha ujenzi kilichotolewa. |
| Masharti kuhusu mabango ya biashara | **14** | (1) | Sheria Ndogo hizi zinatoa katazo kwa mtu yeyote kuweka au kubandika bango la biashara, kuandika maandishi yanayotangaza biashara katika eneo la mamlaka ya halmashauri bila kupata kibali cha halmashauri. |
| | | (2) | Litakuwa ni jukumu la mtu yeyote anayetaka kuweka bango la biashara ndani ya halmashauri kuomba kibali kutoka halmashauri kulingana na **jedwali la tano la sheria Ndogo hizi** na kulipa ada ya bango kwa mujibu wa jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi**.** |
| | | (3) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, halmashauri inayo mamlaka ya kuelekeza sehemu au mahali sahihi pa kuweka au kubandika bango la biashara. |
| | | (4) | Halmashauri ina mamlaka ya kuondoa au kufuta bango la biashara lilowekwa katika mamlaka yake bila kufuata masharti ya Sheria Ndogo hizi. |
| | | (5) | Litakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuondoa bango lililokwishawekwa bila kuomba kibali cha maandishi kwa halmashauri na kukubaliwa kufanya hivyo kwa maandishi. |
| | | (6) | Halmashauri haitaruhusu bango lililokwishawekwa liondolewa, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | isipokuwa endapo sababu zifuatazo zitatolewa na mmiliki wa bango;<br>a) Kufungwa kwa biashara husika,<br>b) Kuhamisha biashara kutoka sehemu moja hadi nyingine,<br>c) Kushindwa kulipa ushuru wa bango husika, sharti isiwe katikati ya mwaka wa fedha,<br>d) Kubadilisha aina ya bango/ biashara. |
| Sehemu ya kuegesha magari | **15** | (1) | Halmashauri imetenga maeneo maalum katika mitaa na kati kati ya mji kuwa sehemu ya kuegesha magari kwa **Mujibu wa jedwali la sita la Sheria Ndogo hizi.** |
| | | (2) | Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuamua idadi ya magari yanayotakiwa kuegeshwa katika kila egesho moja. |
| | | (3) | Kila gari litakaloegeshwa katika maegesho litatakiwa kulipiwa ushuru wa kuegesha magari kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi, Isipokuwa magari yafuatayo hayatatozwa ushuru wa maegesho;<br>a. Magari ya wanadiplomasia,<br>b. Magari ya Serikali,<br>c. Magari ya jeshi,<br>d. Magari ya zimamoto,<br>e. Gari ambalo linamshusha mtu na kuondoka na halikai Zaidi ya dakika tatu.<br>f. Magari yanayofanya usafi katika eneo la halmashauri,<br>g. Magari yaliyoegeshwa katika sehemu za kuabudu wakati wa ibada, |
| | | (4) | Bila kuathiri kifungu cha 15 (3) cha Sheria Ndogo hizi, halmashauri inaweza kusamehe gari lolote kulipa ushuru wa maegesho iwapo itaridhika na sababu zilizotolewa na mwombaji wa msamaha huo. |
| | | (5) | Ushuru wa maegesho utakusanywa siku zote za juma kuanzia saa kumi na mbili asubuhi (12.00) hadi saa kumi nambili za jioni (12.00), bila kujali siku za sikukuu za kitaifa. |
| Maegesho maalum ya malori | **16** | (1) | Halmashauri inaanzisha maegesho maalum ya malori kwa malori yote yanayosafirisha mizigo kupitia eneo la mamlaka ya halmashauri na yanayokusudia kulala au kupumzika kwa muda |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | katika halmashauri kabla ya kuendelea na safari nje ya halmashauri yatatakiwa kuegeshwa katika maeneo maalum yaliyotengwa na halmashauri. |
| | | (2) | Kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi, litakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuegesha lori pembezoni mwa barabara, katika vituo vya kuuzia mafuta, majengo ya watu binafsi, majengo ya mashirika, gereji, maeneo ya wazi na maeneo mengine yote kwa lengo la kulaza au kupumzika kwa muda ili aendelee na safari. |
| | | (3) | Kila lori litakaloegeshwa katika maegesho maalum ya malori yaliyoanzishwa na halmashauri litatozwa ushuru kwa mujibu wa jedwali la kwanza la sheria Ndogo hizi. |
| | | (4) | Malori yote yatakayoingia katika vituo vya kuuzia mafuta hayatatakiwa kusimama katika vituo vya mafuta zaidi ya dakika thelathini. |
| | | (5) | Litakuwa ni kosa kwa dereva yeyote wa lori kuegesha lori analoendesha katika maeneo ambayo hayajaruhusiwa na halmashauri kwa ajili ya maegesho. |
| Vituo vya mabasi | **17** | (1) | Itakuwa marufuku kwa basi lolote kushusha au kupakia abiria na mizigo kinyume na eneo lililoainishwa na halmashauri kuwa ni kituo cha mabasi kwa **mujibu wa jedwali la saba la Sheria Ndogo hizi.** |
| | | (2) | Itakuwa ni marufuku kwa mabasi yanayofanya safari ndani ya halmashauri kukaa katika vituo vya njiani zaidi ya dakika tano baada ya kutoka katika kituo cha mabasi kwa lengo la kushusha na kupakia abiria. |
| | | (3) | Kila basi linaloingia na kutoka katika vituo cha Mabasi vya halmshauri litalazimika kulipiwa ushuru kwa mujibu wa jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi |
| Ushuru wa madini ya ujenzi | **18** | (1) | Halmashauri itatoza ushuru wa madini ya ujenzi yanayozalishwa ndani ya eneo la halmashauri kwa mujibu wa viwango vilivyobainishwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi. |
| | | (2) | Shughuli za Uchimbaji wa madini ya ujenzi zitafanyika katika maeneo yaliyopitishwa na halmashauri kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya ujenzi baada ya kufanya tathmini ya athari ya mazingira. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | (3) | Mtu, Taasisi, Kampuni au kikundi kinachokusudia kuanzisha machimbo ya madini ya ujenzi katika eneo la halmashauri kitatakiwa kuwasilisha maombi kwa Mkurugenzi ili kupata kibali cha kuchimba madini ya ujenzi. |
| | | (4) | Maombi ya kibali yatatakiwa kuambatishwa na taarifa zifuatazo;<br>a) Leseni ya uchimbaji wa madini ya ujenzi iliyotolewa na mamlaka husika,<br>b) Aina ya madini ya ujenzi yanayokusudiwa kuchimbwa,<br>c) Nyaraka za kuthibitisha umiliki wa eneo na ukubwa wa eneo husika,<br>d) Mpango wa utunzaji wa mazingira katika eneo la uchimbaji,<br>e) Uthibitisho wa Muhtasari wa serikali ya Mtaa ambako madini ya ujenzi yatafanyika ukionyesha kukubaliana au kutokubaliana na uchimbaji huo<br>f) Uthibitisho wa kulipa ada ya kibali cha kuchimba madini ya ujenzi kinachotolewa na halmashauri. |
| | | (5) | Mkurugenzi ndani ya muda wa siku saba (7) tangu kupokea maombi,atatakiwa kukagua eneo ambalo uchimbaji wa madini ya ujenzi unakusudia kufanyika ili kujiridhisha iwapo eneo hilo linaafaa kwa shughuli za uchimbaji . |
| | | (6) | Mkurugenzi ndani ya muda wa siku tatu (3) tangu kukamilika kwa ukaguzi wa eneo lililoombewa kibali atatakiwa kukubali au kukataa maombi hayo na endapo atakataa atatakiwa kutoa sababu za kukataa maombai hayo. |
| | | (7) | Usafirishaji wa madini ya ujenzi ndani ya halmashauri utafanyika kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni kila siku. |
| | | (8) | Kila mmiliki wa chombo/gari linalotumika kusafirisha madini ya ujenzi anatakiwa kuhakikisha kuwa chombo/gari linafunikwa wakati wote wa usafirishaji wa madini ya ujenzi. |
| | | (9) | Litakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuchimba madini ya ujenzi katika maeneo ambayo hayajapitishwa na halmashauri kwa ajili ya uchimbaji. |
| Ushuru wa huduma | **19** | (1) | Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kutoka kwa kila mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | (2) | Ushuru wa huduma utatozwa kwa kila mfanyabiashara mwenye lesenikila mwisho wa mwezi baada ya kuwasilisha taarifa zake za mauzo ghafi za mwezi husika kutoka ofisi za mamlaka ya Mapato Tanzania zilizopo katika halmashauri. |
| | | (3) | Ushuru wa huduma utatozwa kwa kiwango kisichozidi 0.3% ya mauzo ghafi yaliyofanyika na mfanyabiashara baada ya kutoa kodi ya ongezeka la thamani (VAT) na ushuru wa forodha. Isipokuwa kwa benki za biashara ushuru wa huduma utatozwa 0.2% ya mauzo ghafi. |
| | | (4) | Kila mfanyabiashara atawajibika kuwasilisha taarifa yake ya mauzo ghafi toka ofisi za mamlaka za mapato kila baada ya kipindi cha mwisho wa mwezi kwa lengo lakupigiwa hesabu ya ushuru wa huduma. |
| | | (5) | Litakuwa ni kosa kwa mfanyabiashara kushindwa kuwasilisha taarifa za mauzo au kuwasilisha taarifa za uongo kwa halmashauri. |
| | | (6) | Mfanyabiashara atakayebainika kufanya kosa kwa mujibu wa kifungu cha 19 (5) atatozwa faini kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na kulipa ushuru unaostahili. |
| Ada ya Kibali cha Sherehe | **20** | (1) | Mtu yeyote mwenye nia ya kufanya sherehe ndani ya halmashauri ni lazima aombe na kupata kibali cha kufanya sherehe kutoka halmashauri kwa mujibu wa **jedwali la nane la Sheria Ndogo hizi** |
| | | (2) | Kibali cha Sherehe kitatolewa baada ya mwombaji kujaza fomu ya maombi kwa Mujibu wa **Jedwali la tisa la Sheria Ndogo hizi.** |
| | | (3) | Mwombaji atapewa kibali husika kwa mujibu wa jedwali la nane la Sheria Ndogo hizi baada ya kukamilisha malipo ya ada husika. |
| | | (4 | Ada ya kibali cha Sherehe italipwa kulingana na viwango vya ada vilivyobainishwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi. |
| Ushuru wa Mazao ya Uvuvi | **21** | (1) | Kila mfanyabaishara wa mazao ya uvuvi ndani ya halmashauri atawajibika kulipa ushuru wa mazao ya uvuvi kwa mujibu wa viwango vilivyobainishwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi. |
| | | (2) | Utakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara anayeingiza mazao ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | uvuvi kutoka nje ya Mkoa kupata kibali toka halmashauri cha kuingiza mazao ya uvuvi ndani ya halmashauri kwa mujibu wa **jedwali la kumi la Sheria la Ndogo hizi.** |
| | | (3) | Ni marufuku kwa mfanyabiashara wa mazao ya uvuvi kuingiza mazao ya uvuvi ndani ya halmashauri bila kulipa ushuru kinyume na Sheria Ndogo hizi. |
| Masharti ya upangaji wa vibanda vya halmashauri | **22** | (1) | Kila Mpangaji wa vibanda/ nyumba ya halmashauri anatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;<br><br>I. Kuhakikisha analipa kodi ya pango kwa kipindi cha miezi mitatu mitatu,<br>II. Kujaza mkataba wa upangajia na halmashauri kabla ya tarehe 01 julai kila mwaka,<br>III. Kuwa na leseni ya biashara iliyotolewa na halmashauri ikiwa hai muda wote.<br>IV. Kutokupangisha kibanda/kuuza kibandakwa mtu mwingine bila idhini ya halmashauri. |
| | | (2) | Litakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kukiuka masharti yaliyowekwa katika kifungu cha 22 (1) cha Sheria Ndogo hizi. |
| Ada ya usajili wa vyombo vya usafiri vya biashara | 23 | (1) | Kila mmiliki wa chombo cha usafiri cha biashara anatakiwa kusajili chombo chake kila mwaka kwa kulipa gharama za usajili kwa mujibu wa jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi. |
| | | (2 | Kila dereva wa chombo cha usafiri cha biashara anatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ;<br>a. Kuwa na leseni ya udereva,<br>b. Kuvaa sare yenye namba mgongoni,<br>c. Kusajili chombo chake kila mwaka tarehe 01 julai,<br>d. Kuhakikisha vyombo vya usafiri vya biashar vitaegeshwa katika maeneo yaliyotengwa,<br>e. Kuhakikisha kila bajaji inakuwa na namba inayoonekana ubavuni, |
| | | (3) | Ni marufuku kwa mmiliki wa chombo cha usafiri cha biashara kuendesha chombo chake bila kusajili kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Makosa na adhabu** | **24** | (1) | Mtu yeyote ambaye;<br>a. Atajenga au kufanya maendelezo yoyote ya ardhi / kiwanja/ukarabati wa jengo bila kibali cha ujenzi<br>b. Atamzuia Afisa muidhiniwa kutekeleza majukumu yake,<br>c. Atamshawishi mtu mwingine au kikundi cha watu kukataa, ma au kukwepa kulipa ada au ushuru,<br>d. Atatoa lugha ya kashfa au kejeli kwa Afisa muidhiniwa au wakala katika utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br>e. Atakataa kutii agizo lolote alilopewa na halmashauri,<br>f. Atakataa kulipa ushuru, ada au kodi zinazotozwa na halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi,<br>g. Ataendesha au kumiliki soko katika eneo la halmashauri bila kibali cha halmashauri,<br>h. Atakwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi,<br>i. Atachimba madini ya ujenzi katika maeneo yasiyopitishwa na halmashauri,<br>j. Atasafirisha madini ya ujenzi kinyume na muda uliotajwa na Sheria Ndogo hizi,<br>k. Ataingiza mazao ya Uvuvi ndani ya halmashauri kutoka nje ya mkoa bila kibali cha halmashauri,<br>l. Ataendesha bajaji au pikipiki bila kuwa na leseni ,<br>m. Ataendesha bajaji au pikipiki bila kuisajili. |
| | | (2) | Mtu huyo atakuwa amekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi, na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi za kitanzania milioni moja 1,000,000/= au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote kwa pamoja kifungo na faini. |
| **Mamlaka ya kufifilisha kosa** | **25** | | Iwapo mtu aliyetenda kosa chini ya Sheria hizi atakiri makosa kabla shauri halikufikishwa mahakamani na kulipa faini kwa hiari, Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa lake baada ya mkosaji kujaza kwa mujibu wa jedwali la kumi la Sheria Ndogo hizi. |
| **Kufutwa kwa** | **26** | | Sheria Ndogo hizi zinafuta sheria zifuatazo za halmashauri’ |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Sheria Ndogo** | | | i. Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka ,2010, Tangazo la Serikali namba 432 ta la tarehe 19/11/2010<br>ii. Sheria Ndogo za Ada na Ushuru (Marekebisho) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka 2022, Tangazo la serikali namba 494 la tarehe 15/7/2022<br>iii. Sheria Ndogo za (Ushuru wa Masoko na Kodi ya vibanda vya biashara) za halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka 2010, tangazo la serikali namba 453 la tarehe 26/11/2010<br>iv. Sheria Ndogo za Ushuru wa Masoko na Kodi ya Vibanda vya biashara (Marekebisho) za halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka 2022, tangazo la serikali namba 493 la tarehe 15/7/2022.<br>v. Sheria Ndogo za (Ushuru wa Vibao vya Matangazo) za halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka 2010, tangazo la serikali namba 431 la tarehe 19/11/2010<br>vi. Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka 2022, tangazo la serikali namba 492 la tarehe 15/7/2022.<br>vii. Sheria Ndogo za (Vibali vya Ujenzi) za halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka 2022, tangazo la serikali namba 488 la tarehe 15/7/2022.<br>viii. Sheria Ndogo za (Ushuru wa huduma) za halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka 2022, tangazo la serikali namba 489 la tarehe 15/7/2022. |

## JEDWALI LA KWANZA

**(Chini ya kifungu cha 4 (1))**

**SEHEMU A.**

**Ada ya Ukaguzi wa nyama (Postmoterm)**

| NA. | Aina ya Mnyama | Kiasi cha Ushuru. |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 1000/= kwa kila Ng'ombe |
| 2 | Mbuzi | 700/= Kwa kila mbuzi |
| 4 | Kondoo | 700/= kwa kila kondoo |
| 5 | Nguruwe | 700/=Kwa kila nguruwe |

**SEHEMU B.**

**Ada ya ukaguzi wa Awali wa mifugo (Antemoterm)**

| NA | Aina ya Mnyama | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Ngo'mbe | 500/= kwa kila Ng'ombe |
| 2 | Mbuzi | 300/= kwa kila Mbuzi |
| 3 | Kondoo | 300/=Kwa kila Kondoo |
| 4 | Nguruwe | 300/= kwa kila nguruwe |

**SEHEMU C.**

**Ada ya Uendeshaji wa Machinjio ya kisasa Tanga**

| NA | Aina ya Mnyama | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 16500/= Kwa Ng'ombe |
| 2 | Mbuzi | 4800/= Kwa mbuzi |
| 3 | Kondoo | 4800/= Kwa kondoo |

**SEHEMU D.**

**Ada katika huduma za Ardhi na Mipango Miji**

| NA | Aina ya huduma | Kiasi cha Ada |
|---|---|---|
| 1 | Kurudia kuonyesha kiwanja mara ya pili/ Kufufua mipaka | 50,000/= Nje ya Mji<br>100,000/= katikati ya Mji |
| 2 | Ombi la kugawa viwanja ili vitoke 2 au Zaidi | 100,000/= |
| 3 | Ombi la kubadili matumizi ya Ardhi | 100,000/= |
| 4 | Ada ya kuweka pingamizi katika Ardhi ( Caveat) | 30,000/= |
| 5 | Ada ya uthibitisho wa nyaraka ( Certification) | 20,000/= |
| 6 | Ada ya uthamini wa uhamisho wa miliki | 1% ya thamani ya kiwanja au nyumba |
| 7 | Ada ya uthamini wa talaka | 40,000/= |
| 8 | Gharama ya kupitisha ramani za vituo vya mafuta | 50,000/= |
| 9 | Tozo ya uthamini kwa taasisi mbalimbali | 3% ya gharama ya kazi ya uthamini |
| 10 | Kibali cha kuweka kibao cha 'NO PARKING' katika eneo la | 30,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| | hifadhi ya barabara | |
| 11 | Ada ya kutafuta nyaraka unazohitaji katika faili ( Search fee) | 40,000/= |
| 12 | Ada ya fomu ya maombi ya kumiliki Ardhi | 20,000/= |
| 13 | Ada ya ramani ya kuonyesha kiwanja | 5000/= kwa ramani |

**SEHEMU E.**
**Ada ya Kusajili Vyombo vya Usafiri vya biashara**

| NA | Aina ya Chombo cha Usafiri | Kiasi cha Ada |
|---|---|---|
| 1 | Gari ya Abiria Zaidi ya 30 | 30,000/= kwa mwaka |
| 2 | Gari ya Abiria chini ya 25 | 20,000/= kwa mwaka |
| 4 | Malori ya mizigo tani 10 na Zaidi | 40,000/= kwa mwaka |
| 5 | Magari ya Mizigo chini ya tani 10 | 30,000/= kwa mwaka |
| 6 | Teksi | 15,000/= kwa mwaka |
| 7 | Bajaji | 22,000/= kwa mwaka |
| 8 | Pikipiki | 17,000/= kwa mwaka |
| | | |

**SEHEMU F.**
**Kodi ya vizimba/ Meza sokoni na Ushuru wa Magenge**

| Na | Aina ya Tozo | Kiasi cha TOZO |
|---|---|---|
| 1 | Kizimba kilichojengwa kwa saruji | 12,000/= kwa mwezi |
| 2 | Kizimba kilichojengwa kwa Mbao | 10,000/= kwa mwezi |
| 3 | Magenge ya biashara yasiyo na sifa za kuwa na Leseni za biashara | 15,000/= kwa kila miezi mitatu |
| 4 | Ushuru wa kufanya biashara sokoni kwa wasio na vizimba | 400/= kwa siku ,na Tshs. 12,000/= kwa Mwezi. |

**SEHEMU G.**
**Ada ya Kukodisha Mali nyingine za Halmashauri.**

| Na | Aina ya mali | Kiasi cha Ada |
|---|---|---|
| 1 | Ukumbi wa halmashauri | 300,000/= kwa siku |
| 2 | Viti | 500/= kwa kiti |
| 3 | Kukodi mtambo wa barabara | 1,000,000/= kwa masaa nane bila gharama za mafuta na bila posho ya dereva. |
| 4 | Kukodi lori | 250,000/= kwa Masaa nane bila poshoya dereva na mafuta. |
| 5 | Bustani ya Manispaa | Ada itategemea bei ya soko na maombi yaliyoombwa katika zabuni husika. |

## SEHEMU H.
## Kodi ya Vibanda vya Halmashauri.

| Na | Eneo kibanda Kilipo | Kodi ya Pango | Kipimo / Muda |
|---|---|---|---|
| 1 | Soko Kuu Songea | 18,000/= | Kwa mita ya mraba moja ,Kwa mwezi, |
| 2 | Manzese “A” | 10,000/= | Kwa mita ya mraba moja,Kwa mwezi, |
| 3 | Manzese “B” | 13,000/= | Kwa mita ya mraba moja, Kwa mwezi, |
| 4 | Stendi ya Mfaranyaki | 18,000/= | Kwa mita ya mraba moja,Kwa mwezi, |
| 5 | Mtaa wa Zanzibar | 8000/= | Kwa mita ya mraba moja,Kwa mwezi, |
| 6 | Soko la Mazao Msamala | 9000/= | Kwa mita ya mraba moja, Kwa mwezi, |
| 7 | Soko la Mshangano | 5000/= | Kwa mita ya mraba moja,Kwa mwezi |
| 8 | Soko la Bombambili | 5000/= | Kwa mita ya mraba moja,Kwa mwezi |
| 9 | Soko la Lizaboni | 5000/=. | Kwa mita ya mraba moja,Kwa mwezi |
| 10 | Soko la Mfaranyaki | 6000/= | Kwa mita ya mraba moja, Kwa mwezi |
| 11 | Soko la Majengo | 6000/= | Kwa mita ya mraba moja,Kwa mwezi |
| 12 | Eneo la Majengo Shuleni | 6000/= | Kwa mita ya mraba moja, Kwa mwezi |
| 13 | Soko la Ruhuwiko | 5000/= | Kwa mita ya mraba moja, Kwa mwezi |
| 14 | Soko la Mjimwema | 5000/= | Kwa mita ya mraba moja, Kwa mwezi |
| 15 | Stendi ya Seedfarm | 5000/= | Kwa mita ya mraba moja, Kwa mwezi |
| 16 | Jengo lililopo eneo la Sido Songea | 18,000/= | Kwa mita ya mraba moja , Kwa mwezi |
| 17 | Eneo la Green Belt | 1000/= | Kwa mita ya mraba moa, Kwa mwezi |
| 18 | Stend ya Tanga | 18,000/= | Kwa mita ya mraba moja, Kwa mwezi |

## SEHEMU I.
## Ada ya Vibali vya Ujenzi/Ukarabati

| Na | Aina ya Jengo | Kiasi cha Ada | Kipimo |
|---|---|---|---|
| 1 | Jengo la Makazi | 250/= | Kwa mita ya mraba moja |
| 2 | Jengo la Biashara | 500/= | Kwa mita ya mraba moja |
| 3 | Jengo la Makazi na Biashara | 350/= | Kwa mita ya mraba moja |
| 4 | Ujenzi wa fensi/ ukuta | 500/= | Kwa kila mita moja ya mzunguko |
| 5 | Ada ya Kuhuisha Kibali cha ujenzi | 50% ya gharama za awali | |
| 6 | Jengo la Ghorofa la makazi | 250/= | Kwa mita ya mraba moja kwa kila sakafu ya ghorofa( floor) |
| 7 | Jengo la Ghorofa ya biashara | 500/= | Kwa mita ya mraba moja, kwa kila sakafu ghorofa (floor) |
| 8 | Jengo la ghorofa na makazi | 350 | Kwa mita ya mraba moja, kwa kila sakafu ghorofa (floor) |

## SEHEMU J.
## Ushuru wa Mabango ya Matangazo

| Na | Aina ya bango / Tangazo | ushuru kwa mwaka | Kipimo |
|---|---|---|---|
| 1 | Bango lisilowaka | 7000/= | Kwa futi ya mraba moja |
| 2 | Bango linalowaka | 10,000/= | Kwa futi ya mraba moja |
| 3 | Maandishi/alama za ukutani | 10,000/= | Kwa futi ya mraba moja |
| 4 | Mabango ya alama za umeme | 10,000/= | Kwa futi ya mraba moja |
| 5 | Bango linaloonesha kitu/ sehemu/madhumuni maalum<br>I. lisilowaka<br>II. linalowaka | 7000/=<br>10000/= | Kwa futi ya mraba moja<br>Kwa futi ya mraba moja |
| 6 | Mabango ya matangazo/ promotion ya muda mfupi | 50,000/= | Kwa kila tangazo |
| 7 | Vipeperushi | 50,000/=<br>50,000/= | Kwa vipeperushi 100 vya mwanzo.<br>Kwa kundi lingine la vipeperushi linalofuata. |
| 8 | Mabango ya kwenye magari | 10,000/= | Kwa futi ya mraba moja. |
| 9 | Mabango ya kwenye magari yanayo tangaza biashara binafsi | 4000/= | Kwa futi ya mraba moja |

## SEHEMU K.

## Ushuru wa Kuegesha Magari

| Na. | Aina ya Gari | Zaidi ya dakika mbili | Zaidi ya saa moja | Kulaza Gari |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Gari ya mizigo chini tani 5 | 1000/= | 1500/= | 2000/= |
| 2 | Gari ya mizigo Zaidi ya tani 5 | 1000/= | 2000/= | 3000/= |
| 3 | Gari ndogo (Luxury) | 1000/= | 1500/= | 2000/= |
| 4 | Bajaji | 500/= | 1000/= | 1500/= |

## SEHEMU L.

## Ushuru wa Kuegesha Malori katika Yadi ya Halmashauri

| Na. | Aina ya Gari | Muda | Kiasi |
|---|---|---|---|
| 1 | Lori | Kwa masaa yasiyozidi masaa sita (6) | 2000 |
| 2 | Lori | Kwa masaa yanayozidi masaa sita (6) | 3000 |
| 3 | Lori | Kulaza gari kwa usiku mmoja | 5000 |

## SEHEMU M.

## Ushuru wa Kupakia na Kushusha Mizigo mjini na Masokoni

| Na. | Ukubwa wa Gari | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Lori/gari la tani 1 hadi tani 4 | 1500/= kila linapopakia na kushusha mizigo |
| 2 | Lori/gari la tani 5 hadi tani 9 | 5000/= kwa kila linapopakia |

| | | |
|---|---|---|
| | | na kushusha mzigo |
| 3 | Lori/gari la tani 10 na kuendelea | 12,000/= kwa kila linapopakia au kushusha mzigo |

**SEHEMU N.**

**Ushuru wa kituo cha Mabasi**

| Na. | Aina ya Gari | Kiwango cha ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Gari au basi laenye uwezo wa kubeba abiria 41 hadi 65 | 3000/= kwa siku |
| 2 | Gari au basi (Min bus) yenye uwezo wa kubeba abiria 18 hadi 40 | 2000/= kwa siku |
| 3 | Gari au hiace yenye kubeba abiria 8 hadi 17 | 1000/= kwa siku |
| 4 | Tax ( Cab taxes) | 1000/= kwa siku |
| 5 | Lori | 1500/= kwa siku |
| 6 | Gari ndogo binafsi | 1000/= kwa siku |
| 7 | Bajaji na pikipiki | 500/= kwa siku |
| 8 | Ushuru wa kuingia stendi bila kuwa na tiketi ya kusafiria. | 200/ kwa siku |

**SEHEMU O.**

**Ushuru wa Madini ya Ujenzi**

| Na. | Aina za Madini | Kiasi cha Ushuru | Kipimo |
|---|---|---|---|
| 1 | Mawe | 1500/= | Kwa mita ya ujazo 1 |
| 2 | Kokoto | 2000/= | Kwa mita ya ujazo 1 |
| 4 | Mchanga | 1500/= | Kwa mita ya ujazo 1 |
| 5 | Moramu/Kifusi/Udongo | 1000/= | Kwa mita ya ujazo 1 |
| 6 | Chokaa | 1000/= | Kwa mita ya ujazo 1 |
| 7 | Madini mengine ya ujenzi | 1000/= | Kwa mita ya ujazo 1 |
| 8 | Kibali cha kuchimba madini ya ujenzi ndani ya Halmashauri | 200,000/= | Kwa kila mchimbaji, kwa mwaka |

**SEHEMU P.**

**Ada za Vibali vya Sherehe/Matamasha**

| Na. | Aina ya Sherehe | Kiasi cha Ada ya kibali kwa siku |
|---|---|---|
| 1 | Harusi, sendoff na Kitchen Party | 50,000/= |
| 2 | Promotion za kibiashara | 100,000/= |
| 3 | Kupiga Muziki wa kibiashara | 50,000/= |
| 4 | Sherehe za uzinduzi wa nyimbo za injili,asili au biashara | 40,000/= |
| 5 | Mashindano ya ngoma za asili | 50,000/= |
| 6 | Sherehe za kipaimara ,birthday, komunyo na Maulid | 20,000/= |
| 7 | Sherehe ya upatu wa kupeana pesa /vitu ( Majamanda) | 30,000/= |
| 8 | Sherehe za mahafali kwa mtu binafsi,shule binafsi na taasisi binafsi | 20,000/= |
| 9 | Kibali cha kufanya matangazo ya nyimbo za injili au mikutano ya injili | 20,000/= |
| 10 | Matangazo ya kumnadi msanii yeyote | 50,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 11 | Kibali cha matangazo ya kuwepo kwa promotion yeyote ya kampuni kutangaza huduma au bidhaa | 50,000/= |
| 12 | Kibali cha kuongeza muda wa kufunga bar/grocery au tamasha la kuuza vileo | 100,000/= |
| 13 | Kibali cha kuuza Vileo masaa 24 | 200,000/= |
| 14 | Kibali cha kufanya matangazo ya msiba | 20,000/= |

**SEHEMU Q.**

**Ushuruwa Mazao ya Uvuvi**

| Na | Aina ya Zao | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Tenga la Samaki/ dagaa wakavu | Tshs. 500/= kwa tenga /boksi/ kiroba/ chombo cha Kg 5 – 10. |
| 2. | Tenga la Samaki/ dagaa wakavu | Tshs. 1,000/= kwa tenga /boksi/ kiroba/ chombo cha Kg 11 – 50. |
| 3. | Tenga la Samaki/ dagaa wakavu | Tshs. 2500/= kwa tenga /boksi/ kiroba/ chombo cha Kg 51 – 100. |
| 4. | Tenga la Samaki/ dagaa wakavu | Tshs. 4,000/= kwa tenga /boksi/ kiroba/ chombo cha Kg 101 – 200. |
| 5. | Tenga la Samaki/ dagaa wakavu | Tshs. 6,000/= kwa tenga /boksi/ kiroba/ chombo cha Kg 201 – 300. |
| 6. | Tenga la Samaki/ dagaa wakavu | Tshs. 10,000/= kwa tenga /boksi/ kiroba/ chombo cha Kg 300 na kuendelea. |
| 7. | Tenga la Samaki wabichi | Tshs. 2,000/= kwa tenga /boksi/ kiroba/ chombo cha Kg 10 – 50. |
| 8. | Tenga la Samaki wabichi | Tshs. 3,000/= kwa tenga /boksi/ kiroba/ chombo cha Kg 51 – 100. |
| 9. | Tenga la Samaki wabichi | Tshs. 5,000/= kwa tenga /boksi/ kiroba/ chombo cha Kg 101 – 200. |
| 10. | Tenga la Samaki wabichi | Tshs. 10,000/= kwa tenga /boksi/ kiroba/ chombo cha Kg 201 – 300. |
| 11. | Tenga la Samaki wabichi | Tshs. 15,000/= kwa tenga /boksi/ kiroba/ chombo cha Kg 301 – 500. |
| 12. | Tenga la Samaki wabichi | Tshs. 20,000/= kwa tenga /boksi/ kiroba/ chombo cha Kg 501 – 1,000. |
| 13. | Gunia la nazi | 3% ya bei ya kununulia |
| 14. | Bidhaa nyingine zote zitokanazo na mazao ya samaki | 3% ya bei ya kununulia |

JEDWALI LA PILI

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

[NEMBO YA HALMASHAURI]

HATI NA. …………………… ….. Tarehe ……………………...

FOMU YA KUKAMATA MALI

*(Chini ya Sheria Ndogo 8(1))*

Mimi ……………………………. ambaye ni Afisa Muidhiniwa nathibitisha kukamata mali zifuatazo;

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

Ambazo zinamilikiwa na Bwana/ Bibi …………………………………………….. leo hii tarehe ……………………. Saa …………………………. Hapa ……………………… (*mahali*) kwa kosa la ……………………………..

Sahihi (Afisa Muidhiniwa) …………………………………….

Mmiliki wa mali

Jina ………………………………..

Sahihi ……………………………..

Tarehe …………………………….

**NB: Fomu hii ijazwe nakala mbili:-**Nakala moja kwa afisa muidhiniwa na nakala ya pili kwa mmiliki wa mali.

JEDWALI LA TATU

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

[NEMBO YA HALMASHAURI]

Hati Na. ………………………………….

Kwa: ……………………………………… (jina la mwombaji)

**KIBALI CHA UJENZI**

(*Chini ya Sheria Ndogo 13 (5).)*

KIBALI HIKI cha ujenzi kimetolewaleo tarehe ………… mwezi ……………….. mwaka ………………….. kwa ……………………………… wa S. L. P …………… kwa ajili wa ……………………………… katika kiwanja Na. ………….. Kitalu ……………… eneo la ………………….. ndani ya mamlaka ya Halmashauri.Kwa sababu Mwombaji amekidhi vigezo na Maharti yote.

……………………… ……………………………

Afisa Mipango miji Mhandisi Ujenzi

Tarehe………………… Tarehe………….

JEDWALI LA NNE

**FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA UJENZI**

*(Chini ya Sheria Ndogo 13(5)*

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA

(NEMBO YA HALMASHAURI)

(Ijazwe na mwombaji)

I. Jina la Mwombaji …………………………………………..
II. Jina La Kampuni/ Shirika/ …………………………………
III. Anuani yake S. L. P. ………… Simu: ……………………Wilaya ………………
IV. Mahali ofisi yake ilipo; Mtaa ……..……. Kata ……… Wilaya …………………
V. Mahali anapotaka kujenga ……………Mtaa …………………kiwanja na.....................Kitalu na.....................................
VI. Ukubwa wa eneo linalojengwa nyumba …………………………………………
VII. Aina ya Makazi……………………………(Makazi,biashara, biashara na makazi,uzio. )

**NATHIBITISHA**: Kuwa maelezo yote niliyotoa hapo juu ni sahihi na kweli.

Jina la mwombaji ………………………………………………………………………

Sahihi ya mwombaji …………………………………………………………………...

Tarehe …………………………………………………………………………………….

Mhuri ……………………………………………………………………………………..

NB; Maombi yaambatane na nyaraka zote muhimu zilizotajwa katika kifungu cha 13 (2) .cha Sheria Ndogo hizi kulingana na aina ya jengo.

JEDWALI LA TANO

FOMU YA MAOMBI YA KUWEKA BANGO LA BIASHARA

Chini ya kifungu cha 14 (2))

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

[NEMBO YA HALMASHAURI]

HATI NA. ……………………….. Tarehe ……………………...

**FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA KUBANDIKA MABANGO YA BIASHARA**

*(Chini ya Sheria Ndogo 14 (2))*

(Ijazwe na mwombaji)

I. Jina la Mwombaji ………………………………………..
II. Jina La Kampuni/ Shirika/ …………………………………
III. Anuani yake S. L. P. ………… Simu: ………… Wilaya ……..
IV. Mahali ofisi yake ilipo; Mtaa ……..……. Kata ……… Wilaya …………………
V. Mahali biashara ilipo ………………Mtaa ……………………………
VI. Namba ya leseni ya biashara ……………………………………………
VII. Idadi ya mabango ya zamani yaliyopo ……………………………………
VIII. Idadi ya mabango mapya yanayotarajiwa kubandikwa ……………………………
IX. Mahali na Idadi ya mabango yatakayobandikwa ………………………………
X. Ukubwa wa mabango ……………………

**NATHIBITISHA**: Kuwa maelezo yote niliyotoa hapo juu ni sahihi na kweli.

Jina la mwombaji ……………………………………………………………………

Sahihi ya mwombaji ……………………………………………………………...

Tarehe …………………………………………………………………………….

Mhuri ……………………………………………………………………………..

Nakala ya kibali itunzwe na mwombaji kwa ajili ya ukaguzi wakati wowote:

Nakala ya kibali hiki itanaki kwa:

a) Afisa Mtendaji wa Mtaa………………………….
b) Afisa Mtendaji Kata ya ………………………….

**JEDWALI LA SITA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**
**(NEMBO YA HALMASHAURI)**
**MAENEO YALIYOTENGWA YA KUEGESHA MAGARI**
**(Chini ya Kifungu cha 15(1))**

| NA | MTAA | JINA LA EGESHO | AINA YA BIASHARA | IDADI YA EGESHO |
|---|---|---|---|---|
| **1** | CCM (old Tanesco- Mpate | Soko kuu | Maegesho | 34 |
| **2** | CCM ( tra – Ruvuma distributor) | Soko kuu | Maegesho | 18 |
| **3** | CCM ( Songea –Mbinga) | Soko kuu | Maegesho | 50 |
| **4** | CCM (NMB bank- NBC bank) | Soko kuu | Maegesho | 30 |
| **5** | Bustani ya manispaa | Bustani ya manispaa | Maegesho | 21 |
| **6** | Mpambalyoto ( NSSF- Magereza) | Nssf | Maegesho | 8 |
| **7** | Mpambalyoto (TTCL-Government Hospital | Ttcl | Maegesho | 4 |
| **8** | Mpambalyoto (DeluxMpambalyoto) | delux/ mtini | Maegesho | 30 |
| **9** | CCM | zanzibar street | Maegesho | 23 |
| **10** | Majimaji (BP station bohari) | Majimaji | Maegesho | 6 |
| **11** | Majimaji (zimanimoto- sovi) | majimaji stadium | Maegesho | 7 |
| **12** | mpambalyoto ( Magereza –st Camilius 1 | Crista park | Maegesho | 12 |
| **13** | Mpambalyoto (Magereza- St Camilius 2 | Crista park | Maegesho | 11 |
| **14** | Quarters ( Sauti- Majengo) | Crista park | Maegesho | 8 |
| **15** | Mwinyimkuu moyo ( yapenda anex-mtoni) | La ChaIz | Maegesho | 15 |
| **16** | CCM ( Mahinya street) | Mahinya | Maegesho | 9 |
| **17** | CCM ( Anglican – Petrol station) | Anglican Church | Maegesho | 12 |
| **18** | Misufini ( Sodeko- Ujenzi | SODECO | Maegesho | 10 |
| **19** | MisufiniI( Kilimomseto- Zimanimoto | SODECO | Maegesho | 12 |

JEDWALI LA SABA

VITUO VYA MABASI

(Chini ya kifungu cha 17(1)

| **Na** | **Jina la kituo cha basi** | **Aina Matumizi** |
|---|---|---|
| 1 | Stendi ya Tanga | Stendi ya Mabasi ya Mkoani |
| 2 | Stendi ya Seedfarm | Kituo cha kususha na Kupakia Abiria |
| 3 | Stendi ya Ruhuwiko | Kituo cha kushusha na kupakia Abiria |
| 4 | Stendi ya Majengo | Stendi ya Mabasi ya vijijini |
| 5 | Stendi ya Mfaranyaki | Stendi ya Daladala |

**JEDWALI LA NANE**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

**(NEMBO YA HALMASHAURI)**

**FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA SHEREHE**
**(Chini ya kifungu cha 20 (1))**

**SEHEMU 'A'**
**(Ijazwe na Mwombaji)**

Majina ya Mwombaji----------------------------wa Sanduku la barua-----------------------Songea.

Kuwasilisha ombi la kibali cha ------------------------------kwa muda wa siku------------------------ shughuli husika itafanyika tarehe-----------------------------hadi tarehe---------------------------- katika mtaa/mitaa ya---------------------------- kata ya---------------------------Manispaa ya Songea.

Nipo tayari kulipa Ada ya Kibali cha kufanya sherehe cha shilingi za kitanzania------------------ kwa siku moja.Hivyo kwa siku (idadi ya siku)------------nitalipa shilingi za Kitanzania--------

Saini ya Mwombaji-------------------------------------------------Tarehe--------------------------------

**SEHEMU 'B'**

**(Kwa matumizi ya Ofisi)**

**UPANDE WA MANISPAA.**

**I**METHIBITISHWA NA ---------------------------------------------------------------------------Afisa Muidhiniwa.

**MAELEKEZO KWA IDARA YA FEDHA YA MANISPAA;** Mwombaji apewe ankra ya malipo kwa shughuli yake ya shilingi za kitanzania-------------------ili niweze kumpa kibali husika.

Saini------------------------------------------Tarehe----------------------------------------

**JEDWALI LA TISA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

**(NEMBO YA HALMASHAURI)**

**KIBALI CHA SHEREHE**
**( Chini ya kifungu cha 20(2))**

Kibali hiki kimetolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa Bi/bw-------------------------- -----------------------wa sanduku la barua -----------------------------------------------------Songea. Kibali hiki kimetolewa leo tarehe -----------------------------------saa---------------------------- kwa ajili ya shughuli ya ---------------------------------------------------------itakayofanyika mtaa wa ------ kata ya -------------------.Kibali kitafanya kazi hadi tarehe---------------------saa-----------.
Masharti ya kibali;

I. Kulipa ada ya kibali hiki kwa mujibu wa Sheria.
II. Kuzingatia muda wa kufanya shughuli husika yaani kuanzia tarehe……………saa…………….hadi tarehe ………………………..saa………
III. Kuzingatia ulinzi , usalama na Afya wa wananchi wakati wa kufanya shughuli husika.

Kibali hiki kimetolewa kwa Mwombaji baada ya kutimiza matakwa ya Sheria Ndogo za ( Ada na Ushuru) za halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka ,2024.
KIBALI HIKI kimesainiwa na -------------------------------------leo tarehe-------------------

Saini-------------------------------------cheo-----------------------------------------

JEDWALI LA KUMI

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

[NEMBO YA HALMASHAURI]

HATI NA. ……………………….. Tarehe ……………………...

**KIBALI CHA KUINGIZA MAZAO YA UVUVI KUTOKA NJE YA MKOA**

*(Chini ya Sheria Ndogo 21(2))*

(Ijazwe na mwombaji)

I. Jina la Msafirishaji…………………………………………..
II. Jina La Kampuni/ Shirika/ …………………………………
III. Anuani yake S. L. P. ………… Simu: …………………… Wilaya ………………
IV. Mahali ofisi yake ilipo; Mtaa ……..……Kata …………. Wilaya ………
V. Namba ya leseni ya biashara ……………………………………………
VI. Eneo mazao ya Uvuvi yanakotoka ………………………………………………
VII. Kiasi cha matenga/Maboksi ya Mazao ya uvuvi kinachokusudiwa kuingizwa halmashauri.
VIII. Kiasi cha Ushuru kinachokusudiwa kulipwa halmashauri kutokana na mzigo……

**NATHIBITISHA**: Kuwa maelezo yote niliyotoa hapo juu ni sahihi na kweli.

Jina la msafirishaji ………………………………………………………………………

Sahihi ya msafirishaji …………………………………………………………………...

Tarehe …………………………………………………………………………………….

Mhuri ……………………………………………………………………………………..

Muda wa kibali hiki ni kuanzia tarehe …………………. Mpaka tarehe ………………………..

Nakala ya kibali itunzwe na mwombaji kwa ajili ya ukaguzi wakati wowote

Nakala ya kibali hiki itanaki kwa:

Afisa Mtendaji wa Kata ya …………………….

__________________________________

Mkurugenzi wa Manispaa/ Afisa Muidhiniwa.

**JEDWALI LA KUMI NA MOJA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

**(NEMBO YA MANISPAA)**

**HATI YA KUKIRI KUTENDA KOSA**

**(Chini ya Kifungu 25)**

Mimi ……………………………………………………..…………………. Nakiri mbele ya Bw/Bi ……………………………………………………. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwambaMnamo tarehe....................... Ya Mwezi ………………………… mwaka ………………………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu namba ……………………………….. Cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka, 2024.

Nipo tayari kulipa kiasi cha faini kinachodaiwa ambacho ni Tshs. ________________________ badala ya kupelekwa Mahakamani, ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha ……….. cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu huku nikifahamu kuwa nilichofanya ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo za ( Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka 2024.

Jina la Mkosaji:____________________________Saini__________________________

Alama ya dole gumba _______________________Tarehe ______________________

**Mbele ya Ushahidi wa.**

Jina_________________________________________________Saini__________________

Alama ya dole gumba ________________________________ Tarehe______________________

Maelezo ya Mkurugenzi _________________________________________________

Jina la Mkurugenzi: __________________________________________________ Saini ya Mkurugenzi: ________________________________________

Tarehe __________________________

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea iligongwa katikaSheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutanowa Baraza la Madiwani wa Halmashauri yaManispaa ya Songea uliofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri tarehe …………. Mwezi …………,2024 na Lakiri hii iligongwa mbele ya:

____________________________________

BASHIR P. MUHOJA,<br>
**MKURUGENZI HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA.**

____________________________________

MICHAEL LEODGAR MBANO,<br>
**MSTAHIKI MEYA HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA.**

NAKUBALI

____________________________________

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)<br>
**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS,**<br>
**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)**

**DODOMA**

TAREHE __________

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)**

**SURA YA 288/2002.**

**SHERIA NDOGO.**

**Zimetungwa chini ya kifungu cha 89.**

**SHERIA NDOGO ZA (KUHIBITIUCHINJAJI HOLELA WA MIFUGO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2024.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jina na tarehe ya kuanza kutumika** | **1.** | | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Kudhibiti Uchinjaji Holela wa Mifugo) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka, 2024 na zitaanza kutumika mara baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali. |
| **Eneo la kutumika** | **2.** | | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea. |
| **Tafsiri** | **3.** | | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:- |
| | | | **"Afisa Muidhiniwa"** Maana yake Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>**"Halmashauri"** Maana yake Halmashauri ya Manispaa ya songea;<br><br>**"Mkurugenzi"** Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea na ni pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi,<br><br>**'Mifugo'**maana yake ni wanyama wote wanaofugwa na binadamu na wanaotakiwa kuchinjwa katika machinjio kama vile Ng'ombe, mbuzi, kondoo, Nguruwe,na kadharika.<br><br>**"Machinjio"** maana yake ni sehemu au eneo maalum liliyotengwa/au kujengwa na halmashauri kwa ajili kuchinjia wanyama.<br><br>**"Wakala"** Ina maana ya mtu binafsi, kikundi cha watu, Kampuni, Taasisi, Shirika au Serikali ya Mtaa atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi' |
| **Uanzishaji wa utaratibu maalum wa uchinjaji wanyama** | **4.** | (1) | Halmashauri imeanzisha utaratibu maalum wa uchinjaji mifugo ndani ya mamlaka ya halmashauri. |
| | | (2) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, mifugo yote inayotakiwa kuchinjwa ndani ya Halmashauri itachinjwa katika machinjio maalum zilizojengwa au kutengwa na halmashauri kwa mujibu wa Jedwali la |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | "A" la sheria Ndogo hizi. |
| | | (3) | Kila mtu anayetaka kuchinja mifugo ndani ya halmashauri anawajibika kufanya hivyo katika machinjio maalum ndani ya halmashauri. |
| | | (4) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Kila mifugo inayotakiwa kuchinjwa ndani ya halmashauri itachinjwa katika machinjio maalum za halmashauri. |
| **Wajibu wa kuchinja katika eneo maalum** | **5.** | (1) | Utakuwa ni wajibu wakila mtu ndani ya halmashauri anayetaka kuchinja mifugo, kuhakikisha anafanya hivyo kwa kutumia machinjio zilizoanzishwa na halmashauri na sio vinginevyo. |
| | | (2) | Ni kosa kwa mtu yeyote kuchinja mifugo yake kinyume na utaratibu ulioelezwa katika kifungu cha 5(1); |
| **Wajibu wa halmashauri** | **6.** | (1) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, halmashauri inao wajibu wa kisheria kuhakikisha inakuwa na machinjio maalum ya kuchinjia mifugo mbalimbali ndani ya mamlaka yake. |
| | | (2) | Halmashauri ina wajibu wa kisheria kuhakikisha huduma zote muhimu katika machinjio zinapatikana ili kurahisisha uchinjaji wa mifugo katika machinjiondani ya mamlaka ya Halmashauri. |
| **Machinjio za watu binafsi** | **7.** | (1) | Itakuwa ni kosa kwa mtu au taasisi binafsi kumiliki machinjio ndani ya halmashauri bila kuwa na kibali cha halmashauri. |
| | | (2) | Kwa mujibu wa sheria ndogo hizi, halmashauri inayo mamlaka ya kufungia machinjio yoyote ndani ya halmashauri ambayo imeanzishwa kinyume na sheria za nchi ikiwepo kuanzishwa katika maeneo ambayo sio rafiki kwa afya ya binadamu. |
| **Wajibu wa kulipa ada ndani ya machinjio** | **8.** | | Utakuwa ni wajibu kwa kila mtu anayetumia machinjio kuhakikisha anafuata masharti yote yaliyowekwa katika machinjio ikiwepo kulipa ada zote zinazotakiwa kulipwa katika machinjio. |
| **Uteuzi wa Wakala /Afisa muidhiniwa** | **9.** | (1) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Halmashauri inaweza kumteua Wakala kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi; |
| | | (2) | Wakala atakayeteuliwa na Halmashauri atakuwa na jukumu la kuhakikisha matakwa ya Sheria Ndogo hizi yanatekelezwa na kutoza faini kwa niaba ya Halmashauri kama ilivyoelezwa na Sheria hizi; |
| **Uanzishwaji wa Vituo vya ukaguzi** | **10.** | (1) | Halmashauri inaweza kuanzisha Vituo mbalimbali ndani ya Halmashauri kwa madhumuni ya kukagua |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **wa nyama** | | | nyama ndani ya mamlaka ya Halmashauri ili kujiridhisha na eneo ilipochinjwa mifugo hiyo. |
| | | (2) | Ukaguzi wa nyama Vituoni utahusisha uhakiki wa nyaraka mbalimbali zinazotolewa katika machinjio za halmashauri na alama za ukaguzi za kitaalam. |
| | | (3) | Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 10 (1) cha Sheria Ndogo hizi, halmashauri inaowajibu wa kisheria kufanya ukaguzi katika mabucha yote ndani ya halmashauri ili kujiridhisha endapo nyama inayouzwa imezingatia matakwa ya Sheria Ndogo hizi. |
| **Usafirishaji wa mazao ya wanyama** | **11.** | (1) | Kila msafirishaji wa nyama ndani ya mamlaka ya Halmashauri ahakikishe anapata nyaraka muhimu za mzigo wake kama ifuatavyo:-<br>a) Stakabadhi za malipo ya ukaguzi wa nyama kutoka katika machinjio,<br>b) Kuhakikisha nyama anayosafirisha imekaguliwa na afisa mifugo na kugongwa mhuri maalum wa ukaguzi. |
| | | (2) | Ni kosa kwa msafirishaji yeyote wa nyama ndani ya mamlaka yaHalmashauri kusafirisha nyama bila kuzingatia masharti ya kifungu cha 11(1) cha Sheria Ndogo hizi. |
| **Makosa na adhabu** | **12.** | (1) | Mtu yeyote ambaye:-<br>a) Atauza nyama bila kukaguliwa na wataalam wa mifugo,<br>b) Atachinja mifugo eneo tofauti na machinjio za halmashauri<br>c) Atakwepa kwa makusudi kutumia machinjio za halmashauri,<br>d) Ataanzisha machinjio binafsi kinyume na Sheria,<br>e) Atasafirisha nyama bila ya kuwa na nyaraka na alama zilizoelezwa katika kifungu cha 11(1), (a) (b),<br>f) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukiuka matakwa ya Sheria Ndogo hizi<br>g) Atakataa au kushindwa kutii maagizo ya Afisa Muidhiniwa au Wakala,<br>h) Atamzuia Afisa Muidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake,<br>i) Atatishia uhai wa wakala au Afisa Muidhiniwa wakati akitekeleza majukumu yake,<br>j) Atalazimisha kupita katika Vituo vya ukaguzi wa nyama kwa nguvu bila kukaguliwa,<br>k) Atauza nyama buchani ambayo mfugo husika umechinjwa kiholela au kutokaguliwa na Afisa mifugo,<br>l) Siyo msemaji wa Halmashauri, atatangaza hadharani kuwazuia watu wengine wasitekeleze |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | matakwa ya Sheria Ndogo hizi, |
| | | (2) | Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na atashtakiwa mahakamani akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi za kitanzania mia mbili elf utu (200,000/=) na isiyozidi shilingi za Kitanzania milioni moja tu (**1,000,000/=)** au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja; |
| | | (3) | Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kifungu cha 12 (2) cha Sheria Ndogo hizi, Halmashauri inaweza kutaifisha na kuteketeza nyama ya mnyama aliyechinjwa bila kufuata masharti ya Sheria Ndogo hizi. |
| | | (4) | Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteketeza nyama iliyotaifishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 12(3) cha Sheria Ndogo hizi, endapo tu itajiridhisha kuwa mnyama aliyechinjwa hakuzingatia matakwa ya Sheria Ndogo hizi.. |
| | | (5) | Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea kwa mtu yeyote ambaye nyama yake imetaifishwa, kwa kutekeleza mamlaka yake ya kuteketeza nyama hiyo. |
| **Kufifilisha kosa** | **13.** | | Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote yule endapo mkosaji, atakiri kosa lake kwa maandishi kwa kujaza fomu namba1 ya Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini. |

## JEDWALI ''A''

## MACHINJIO ZINAZOTAMBULIKA
**(Chini ya kifungu cha 4(2))**

| NA. | JINA LA MACHINJIO/KARO | AINA YA MIFUGO INAYOCHINJWA |
|---|---|---|
| (i) | Machinjio ya Kisasa ya Tanga | Ng'ombe,Mbuzi na Kondoo |
| (iii) | Karo ya kuchinjia Mifugo Ruvuma | Mbuzi |
| (iv) | Karo ya Kuchinjia Mifugo Lizaboni | Nguruwe |
| (v) | Karo ya kuchinjia Mifugo Lizaboni | Mbuzi |
| (vi) | Karo ya kuchinjia Mifugo Lilambo | Nguruwe |
| (vii) | Karo ya kuchinjia Mifugo Mletele | Nguruwe |
| (viii) | Karo ya kuchinjia mifugo Mjini | Nguruwe |
| (ix) | Machinjio ya Msamala | Nguruwe |

**FOMU NAMBA 1**

**HATI YA KUKIRI KWA HIARI KUTENDA KOSA.**
**(Chini ya kifungu cha 13).**

Mimi:__________________________nakiri mbele ya Bw/Bi:______________Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwamba mnamo tarehe:_______________ya mwezi_________mwaka___________nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu namba__________________cha Sheria Ndogo za **(KudhibitiUchinjaji Holela wa Mifugo**) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea, za mwaka 2024.

Nipo tayari kulipa kiasi cha faini kinachodaiwa ambacho ni Tshs_______________badala ya kupelekwa Mahakamani ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamalaka aliyopewa chini ya kifungu cah 13 cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwahiari yangu kadri ya ufahamu wangu huku ni kifahamu kuwa nilichofanya ni kosa kwa mujibu wa Sheira Ndogo za **(Kudhibiti Uchinjaji Holela wa Mifugo)** za Halmashauri ya Manispaa ya Songea, za mwaka 2024.

Jina la Mkosaji:_________________________saini_____________alama ya dole gumba _____________________________________tarehe________________________________

**Mbele ya Shahidi:**

Jina:________________________________Saini_________________________Alama ya dole gumba:___________________________tarehe:_______________________________________

Maelezo ya Mkurugenzi kwa kifupi:-

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

Jina la Mkurugenzi:______________________________________________________________

Saini ya Mkurugenzi:_____________________________________________________________

Tarehe:_________________________________________________________________________

Mhuri:__________________________________________________________________________

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea iligongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuata azimio laMkutano wa Baraza la Madiwani ulioketi Ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songeatarehe **________________**mwezi**____________**mwaka, 2024, na kushuhudiwa na:-

_____________________________________<br>
BASHIR P. MUHOJA,<br>
**MKURUGENZI HALMASHAURI YA MANISPAA**<br>
**SONGEA.**

___________________<br>
MICHAEL LEODGAR MBANO<br>
MSTAHIKI MEYA, HALMASHAURI YA MANISPAA<br>
**SONGEA.**

**NAKUBALI**

______________________<br>
MOHAMED OMARY MCHENGERWA (**MB),**<br>
**WAZIRI WA NCHI-OFISI YA RAIS,**<br>
**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA).**

**DODOMA**<br>
**Tarehe:____________________**

**Tangazo la Serikali Na ….…………….. La Tarehe………….**

**SHERIA YA SERIKALI ZAMITAA (MAMLAKA ZA MIJI)**

**SURA YA 288**

**(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 89 (1)**

# SHERIA NDOGO ZA (UPULIZIAJI VIUATILIFU) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA, 2024

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jina** | **1.** | | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (**Upuliziaji Viuatilifu)** za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka 2024 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. |
| **Matumizi** | **2.** | | Sheria Ndogo hizizitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Manispaa ya Songea. |
| **Tafsiri** | **3.** | | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itahitajika vinginevyo:-<br><br>‘**Afisa Muidhiniwa’** maana yake ni Afisa Afya yoyote wa halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>**‘Afya’**maana yake ni ukamilifu wa mwili, kiakili na kijamii.<br><br>**“Halmashauri**” Maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Songea.<br><br>**‘Jengo’** maana yake ni jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na halmashauri litumike kwa kuishi, ofisi, shule, taasisi au la kuhifadhia bidhaa mbalimbaliau nyumba za kulala wageni.<br><br>‘**Kiuatilifu’** maana yake ni kemikali/sumu inayotumika kuua wadudu, wanyama au magugu katika nyumba za kuishi, maghala ya kuhifadhia bidhaa na kwenye mazalia mbalimbali ya wadudu wadhulifu na wasumbufu.<br><br>“**Mkurugenzi**’’ Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.<br><br>“**Tilifu”** maana yake ni mdudu, mnyama, magugu au kiumbe chochote kinachodhuru kiumbe kingine.<br><br>“**Wakala/Mzabuni”** maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au taasisi yenye vibali na leseni ya kufanya zoezi la upuliziaji viuatilifu kwa mujibu wa Sheria na kanuni za afya. |
| **Kuanzisha utaratibu wa kupulizia** | **4.** | (1) | Katika kutekeleza azma ya kuboresha afya kwa jamiikatika Halmashauri. Halmashauri inaanzisha utaratibu wa kusimamia upuliziajiviuatilifu katika |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **viuatilifu** | | | majengoyote ndani ya halmashauri. |
| | | (2) | Kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Kila mmiliki wa jengo anatakiwa kufanya upuliziaji wa viuatilifu katika jengo lake angalau mara moja kila mwaka ili kujikinga wa wadudu wadhulifu. |
| | | (3) | Kila mmiliki wa jengo kabla ya kupulizia viuatilifu katika jengo lake atalazimika kujaza fomu maalum ya maombi ya kufanya upuliziaji kwa mujibu wa jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi |
| | | (4) | Kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Mmiliki wa jengo anaweza kupulizia kiuatilifu katika jengo lake kwa kupitia Mzabuni yeyote aliyefanya nae makubaliano na mwenye sifa ya kufanya kazi hiyo. |
| | | (5) | Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 4(3), mmiliki wa jengo hataruhusiwa kufanya upuliziaji wa viuatilifu ndani ya halmashauri bila kufuata utaratibu na kupata kibali cha halmashauri kwa mujibu wa jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi. |
| **Ukaguzi wa jengo kabla ya upuliziaji** | **5** | (1) | Baada ya kupokea maombi ya Upuliziaji kupitia fomu ya Sheria Ndogo hizi, afisa muidhiniwa atatakiwa kufanya ukaguzi wa jengo ili kujua ukubwa wa jengo na aina ya tilifu wanaotakiwa kuuawa. |
| | | (2) | KwaMujibu wa Sheria Ndogo hizi,endapo jengo litapuliziwa na Afisa mudhiniwa wa halmashauri, mmiliki wa jengo atalazimika kulipa shilingi 100 ya kitanzania kwa kila mita ya mraba moja ya eneo linalotakiwa kupuliziwa. |
| | | (3) | Mmiliki wa jengo atalazimika kulipa halmashauri shilingi elfu hamsini tu (50,000/=) kwa kila jengo la mtu binafsi na shilingi laki moja tu (100,000/=) kwa kila jengo la taasisi ikiwa ni ada ya kibali, endapo upuliziaji utafanywa na Mzabuni. |
| | | (4) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, suala la kupulizia viuatilifu katika majengo litakuwa ni lazima kwa kila mmiliki wa jengo katika halmashauri kwa lengo la kujikinga na wadudu wadhulifu. |
| **Matumizi ya wakala** | **6** | (1) | Halmashauri inaweza kumtumia wakala /mzabuni kufanya kazi ya kupulizia viuatilifu katika eneo fulani ndani ya Halmashauri. |
| | | (2) | Endapo mzabuni atatumika kufanya zoezi la upuliziaji viuatilifu katika eneo Fulani ndani ya halmashauri, zoezi la kujaza fomu ya maombi litafanywa na mzabuni husika badala ya mmiliki wa jengo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | (3) | Wakala/mzabuni aliyetafutwa na halmashauri atalazimika kulipa halmashauri 20% ya fedha atakayolipwa na wamiliki wa majengo kutokana na zoezi la upuliziaji viuatilifu lililofanyika katika eneo husika. |
| | | (4) | Itakuwa ni lazima kwa kila mmiliki wa jengo kulipa gharama za upuliziaji wa viuatilifu katika jengo kulingana na viwango vitavyokuwa vimekubaliwa kati ya halmashauri,wakala/mzabuni na wamiliki wa majengo. |
| **Muda wa upuliziaji na utoaji wa cheti** | **7** | (1) | Kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi,Upuliziaji wa viuatilifu unatakiwa kufanyika kuanzia saa 12.00 asubuhi mwisho saa5.00 asubuhi ili kumkinga mpuliziaji asipatwe na viuatilifu katika mwili wake. |
| | | (2) | Baada ya zoezi la upuliziaji kukamilika mmiliki wa jengo atapewa cheti na halmashauri cha kuthibitisha upuliziaji wa viuatilifu katika jengo lake kwa mujibu wa Jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi. |
| **Vifaa vya upuliziaji** | **8** | | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Mpuliziaji ni sharti atumie pampu za upuliziaji viuatilifu ambazo zimethibitishwa na shirika la Afya duniani ambazo zina uwezo wa kutoa vipimo vyenye msukumo wa 55 hadi 65 kwa sekunde. |
| **Vifaa kinga** | **9** | | Katika kipindi chote cha kutekeleza zoezi la upuliziaji, Mpuliziaji ni sharti avae vifaa kinga kama vileovalori, buti (viatu virefu), mipira ya mikononi, kofia ngumu, miwani na barakoa. |
| **Utaratibu wa tozo na malipo ya upuliziaji** | **10** | (1) | Malipo yote yatafanyika katika halmashauri baada ya kupewa ankra ya malipo (Control number) kabla ya kulipa. |
| | | (2) | Mmiliki wa jengo sharti akabidhiwe stakabadhi ya malipo aliyofanya ili kuthibitisha kiasi cha fedha kilicholipwa kwa halmashauri. |
| **Wajibu wa mmiliki wa jengo** | **11** | (1) | Kila mmiliki wa jengo anayetaka kupulizia viuatilifu katika jengo lake, atalazimika kufuata matakwa ya Sheria Ndogo hizi. |
| | | (2) | Litakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kwa mmiliki yeyote wa jengo kufanya zoezi la upuliziaji viuatilifu katika jengo lake kinyume na matakwa ya Sheria Ndogo hizi. |
| **Wajibu wa Afisa Muidhiniwa** | **12** | (i) | Afisa muidhiniwa atakuwa na wajibu wa kuhakikisha yafuatayo;.<br>a) Ahakikishe kwamba anatunza orodha halisi ya wamiliki wa majengo waliofanya upuliziaji katika majengo yao.<br>b) Anachukua hatua za kisheria kwa wamiliki wote wa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Majengo watakaobainika kufanya upuliziaji wa majengo yao bila kufuata matakwa ya Sheria Ndogo hizi.<br>c) Anasimamia kwa jumla zoezi zima la upuliziaji viuatilifu katika majengo ndani ya halmashauri. |
| **Makosa** | **13** | (1) | Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizikwa mtu yeyote:-<br>a) Kufanya upuliziaji wa viuatilifu katika jengo lake bila kufuata masharti ya Sheria Ndogo hizi<br>b) Kukataa kulipa tozo au malipo ya halmashauri kulingana na matakwa ya Sheria Ndogo hizi.<br>c) Kumshawishi mtu mwingine hadharani kutofuata matakwa ya Sheria Ndogo hizi.<br>d) Kumzuia Afisa Muidhiniwa asitekeleze majukumu yake kwa<br>Mujibu wa Sheria Ndogo hizi.<br>e) Kutoa maneno ya kashfa au kejeli kwa Afisa yeyote anayetekeleza matakwa ya Sheria Ndogo hizi.<br>f) Kutoa taarifa za upotoshaji juu ya taratibu zinazotakiwa kufuatwa na mmiliki wa jengo kabla ya kufanya upuliziaji wa viuatilifu katika jengo lake kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi.<br>g) Atashindwa kutii sharti lolote lililowekwa na Sheria Ndogo hizi.<br>h) Atashindwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br>i) Atafanya upuliziaji wa viuatilifu katika jengo lake bila kupata kibali na kukaguliwa na halmashauri. |
| **Adhabu.** | **14.** | (1) | Mtu yeyote atakayetenda kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hizi na akapatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote kwa pamoja yaani faini na kifungo. |
| **Uwezo wa Mkurugenzi** | **15.** | (1) | Mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kumteua Afisa yeyote wa Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi |
| | | (2) | Bila kuathiri kifungu cha 15(1) ya Sheria Ndogo hizi, Afisa yeyote wa Halmashauri atakuwa ni msimamizi wa Sheria Ndogo hizi. |
| | | (3) | Mkurugenzi au Afisa Muidniniwa anaweza kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa na kukiri kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum kwa Mujibu wa jedwali la nne la Sheria Ndogo hizi. |
| **Uwezo wa kuteua wakala** | **16.** | | Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuteua wakala kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo hizi kwa niaba yake itakavyoona inafaa kufanya hivyo. |

**JEDWALI LA KWANZA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

**( NEMBO YA HALMASHAURI)**

**FOMU YA MAOMBI YA KUFANYA UPULIZIAJI VIUATILIFU KATIKA JENGO.**
**( KIFUNGU 4(2) ).**

**SEHEMU YA KWANZA**

**MAELEZO NA ANUANI YA MWOMBAJI**

Jina la Mwombaji…………………………..SLP…………………………

Namba ya Usajili ya Mwombaji…………………………………………

Jina la Mpuliziaji……………………………………………………….

Sifa ya Mpuliziaji……………………………………………………….

**SEHEMU YA PILI**

**ENEOJENGO LILIPO**

Jina la Mmiliki wa jengo linalopuliziwa……………………………………………..

Jengo lipo Mtaa wa …………………………….Kata ya …………………Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Mkoa wa Ruvuma.

**SEHEMU YA TATU.**

**TILIFU WANAOKUSUDIWA KUANGAMIZWA**

Taja aina ya Wadudu unaokusudia kuwaangamiza……………………………………

**SEHEMU YA NNE**

**VIUATILIFU NA VIFAA VINAVYOKUSUDIWA KUTUMIKA**

Viuatilifu vinavyotakiwa……………………………………………………………….

Vifaa vinavyotakiwa…………………………………………………………………

**JEDWALI LA PILI**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

**( NEMBO YA HALMASHAURI)**

**KIBALI CHA KUFANYA UPULIZIAJI VIUATILIFU KATIKA JENGO.**
**( KIFUNGU 4(5) )**

Hii ni kuthibitisha kwamba Bw/Bi…………………………………………………..amefuata taratibu zote kwa Mujibu wa Sheria Ndogo za (Upuliziaji Viuatilifu) za halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka……………..

Ameruhusiwa kufanya zoezi la upuliziaji Viuatilifu katika majengo yake yaliyopo katika kiwanja na………………………………….kitalu……………………………..eneo la…………………………………… ndani ya halmashauri ya Manispaa ya Songea na amelipia ada ya kibali (***Ambatanisha stakabadhi ya malipo na kibali hiki)***.

*Kibali hiki kitafanya kazi kwa muda wa siku thelathini tu kuanzia leo …………..mwezi……………..mwaka …………………………..*

……………………………………………………..

Afisa Afya wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea

JEDWALI LA TATU

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA

(NEMBO YA HALMASHAURI)

**CHETI CHA KUTHIBITISHA KUFANYA UPULIZIAJI VIUATILIFU KATIKA JENGO**

(Chini ya kifungu cha 6(2)).

Hii ni kuthibitisha kuwa Bi/Bw…………………wa Mtaa………………Kata ya ………Halmashauri ya Manispaa ya Songea.Amefanya zoezi la upuliziaji wa Viuatilifu katika jengo lake lililoko kiwanja na………………kitalu………………ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

Upuliziaji huu wa Viuatilifu umefanyika baada ya kuthibitishwa na kusimamiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa Mujibu wa Sheria Ndogo za **(Upuliziaji Viuatilifu )** za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka 2024, leo……………….Mwezi……………….Mwaka……

……………………………………

Afisa Afya wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea

**JEDWALI LA NNE**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

**(NEMBO YA HALMASHAURI)**

**KIFUNGU CHA 15 (3)**

**HATI YA KUKUTWA NA MACHUKIZO**

Mimi …………………………………Nakiri mbele ya Bw/Bi ……………………………………………….. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwamba Mnamo tarehe...................... ya Mwezi ………………………… mwaka ………………………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu namba ……………………………….. Cha Sheria Ndogo za (Upuliziaji Viuatilifu) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka, 2024.

Nipo tayari kulipa kiasi cha faini kinachodaiwa ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 15(3) cha Sheria Ndogo hizo.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Jina: …………………………………….. Saini ………………………………………………

Alama ya dole gumba …………………………………Tarehe ………………………………

**Mbele ya Ushahidi wa.**

Jina: ………………………………………… Saini …………………………… Alama ya dole gumba ………………………………….. Tarehe …………………………….

Maelezo Mafupi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa……….. ………………………

Jina laMkurugenzi …………………………… Saini ………………… Tarehe ………………

Lakiri ya Halmashauri yaManispaa ya Songea imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatiaazimio lililopitishwakwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea tarehe____________ Mwezi ______________,2024 na kubandikwa mbele ya;

BASHIR P. MUHOJA

**MKURUGENZI HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA.**

MICHAEL LEODGAR MBANO

**MSTAHIKI MEYA HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA.**

NAKUBALI

……………………………………

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)

**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS,**

**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITA)**

**DODOMA**

TAREHE …..../………./…….

Tangazo la Serikali Na. __________ La Tarehe ____________

**SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA**

**(SURA YA 290)**

**SHERIA NDOGO.**

**Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1)na 16 (1)**

# SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA, 2024.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jina la Sheria Ndogo | 1. | | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za Mwaka, 2024 |
| Matumizi | 2. | | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote yaliyo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea na zitaanza kutumika kuanzia tarehe ya kutangazwa katika gazeti la Serikali. |
| Tafsiri | 3. | | Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:- |
| | | | **Afisa Mwidhiniwa"** ni Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>**"Halmashauri"** Maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Songea.<br><br>''**Daftari la Wageni"** Maanayake ni kitabu maalum kilichoandaliwa na Halmashauri na kuuzwa kwa mmiliki kwa lengo la kusajili na kutunza kumbukumbu za wageni wanaolala kwenye nyumba ya kulala wageni au hoteli. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | **'Gharama za malazi''** Maana yake ni kiasi cha fedha kinachotozwa na mmiliki wa nyumba za kulala wageni kwa mtu ambaye anapata huduma ya malazi.<br><br>''**Mkurugenzi''** maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea au Afisa yeyote aliyekaimishwa ofisi hiyo akitekeleza majukumu ya Mkurugenzi.<br><br>**"Hoteli"**maana yake ni jengo lililojengwa kwa ajili ya kupokea na kulaza wageni kwa lengo la kupata faida na haitajumuisha jengo lenye vyumba chini ya sita (6), lakini pia haitajumuisha mabweni na nyumba za mapumziko za serikali.<br><br>"**Nyumba ya Kulala Wageni"** maana yake ni jengo lililojengwa kwa ajili ya wageni kwa lengo la kupata faida ambayo itajumuisha jengo ambalo lina vyumba vya kulala wageni visivyopungua sita (6) vinavyotumika kutoa huduma ya vyumba vya kulala, tafsiri hii haitajumuisha nyumba za mapumziko za serikali.<br><br>**"Mgeni"** maana yake ni mtu yeyote ambaye hulipa pango la kukaa kwenye chumba cha kulala wageni, aidha, kwa siku nzima au sehemu ya siku nzima.<br><br>**"Mmiliki"** maana yake ni mtu yeyote anayemiliki kihalali nyumba ya kulala wageni au hoteli na inajumuisha mtu yeyote aliyepewa na mmiliki jukumu la kusimamia Nyumba ya kulala wageni au |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Hoteli au Mwajiriwa au mtu yeyote anayehusika kukusanya gharama za pango toka kwa mgeni kutokana na mgeni huyo kulala kwenye nyumba hiyo ya kulala wageni.<br><br>**'Ushuru'** maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kutokana na nyumba za kulala wageni. |
| Kiwango cha Ushuru | **4.** | (1) | Halmashauri itatoza ushuru wa Nyumba za kulala wageni au Hoteli kwa kila mmiliki wa nyumba za kulala wageni/ hoteli, ushuru ambao utakuwa sawa na asilimia kumi (10%) ya mauzo ya siku kwa kila chumba au vyumba vilivyolaza wageni. |
| | | (2) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, ushuru wa nyumba za kulala wageni /Hoteli utakusanywa na Halmashauri kila mwisho wa mwezi. |
| | | (3) | Malipo yote ya ushuru yatafanyika kwa Halmashauri baada ya ukaguzi wa daftari la Wageni na baadae mmiliki kupewa ankra ya malipo (Control number) kwa ajili ya malipo ya ushuru wa mwezi husika na baadae kupewa stakabadhi ya kieletroniki ya malipo na halmashauri. |
| | | (4) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, siku za ukaguzi wa daftari la wageni itakuwa kati ya tarehe 1 hadi tarehe 7 ya kila mwezi, |
| Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa kufanya | **5** | (1) | Katika utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi, Afisa Mwidhiniwa atakuwa na wajibu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| ukaguzi | | | ufuatao';<br>a. Kukagua nyumba ya kulala wageni/Hoteli kwa lengo la kuhakiki endapo wageni wote waliolala katika vyumba wameorodheshwa katika daftari la wageni.<br>b. Kukagua endapo mmiliki au mtunza nyumba ya kulala wageni/hoteli anacho na anatumia ipasavyo kitabu kilichotolewa na Halmashauri kusajili wageni waliolala katika nyumba yake.<br>c. Kukagua na kuhakiki endapo taratibu zinazosimamia nyumba za kulala wageni/ hoteli zinafuatwa na mmiliki husika.<br>d. Kukagua na kutaka kujua endapo mapato ya ushuru yanayolipwa na mmiliki wa Nyumba ya kulala wageni/ hoteli yanaendana na hali halisi ya mapokezi ya wageni,<br>e. Kukagua endapo nyumba ya kulala wageni/ hoteli ipo katika hali ya usafi.<br>f. Kukagua endapo kwenye vyumba vya kulala wageni kuna mahitaji yote ya msingi na lazima yanayotakiwa kuwepo na<br>g. Kukagua endapo Nyumba ya kulala wageni/hoteli inafanya kazi iliyokusudiwa. |
| | | (2) | Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kifungu cha 5 (1) hapo juu, Halmashauri inaweza kuunda timu maalum ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | wataalam katika kutekeleza majukumu yaliyobainishwa katika kifungu cha 5(1) (a-g) hapo juu. |
| Masharti ya mmiliki/ mtunza Hoteli | 6 | | Kila mmiliki au mtunza hoteli au nyumba ya kalala wageni atahakikisha yanatekelezwa/ yanafanyika;<br>a) Kila mgeni anasajiliwa kwenye daftari la wageni kwa kuingiza taarifa zake zote muhimu bila kujali muda aliokitumia chumba,<br>b) Kitanda kimoja hakitumiki wa wageni wawili au Zaidi wa jinsi moja,<br>c) Kulipa ushuru wa nyumba ya kulala wageni/ hoteli kwa halmashauri ndani ya siku saba (7) baada ya mwezi husika wa mauzokuisha.<br>d) Kulipa ada ya leseni ya biashara ya Nyumba ya kalala wageni/hotel ndani ya muda uliowekwa kwa Mujibu wa Sheria.<br>e) Kuhakikisha kuwa Nyumba ya kulala wageni/ hoteli inakuwa safi muda wote na masharti mengine ya usafi yanafuatwa..<br>f) Kuweka wazi vitabu vya kumbukumbu za wageni na nyaraka zingine wakati waukaguzi.<br>g) Kuweka eneo la wazi leseni ya biashara ya Nyumba ya kulala wageni na kuzingatia masharti kama yalivyo fafanuliwa kwenye Sheria ya Leseni na miongozo mingine ya Kisheria. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | h) Kutoa ushirikiano wa kutosha kwa halmashauri pamoja na Maafisa mbalimbali wa Serikali wakati wote wa kufanyika kwa ukaguzi wa aina yoyote. |
| Wajibu wa mmiliki/ mtunza hotel/nyumba ya kulala wageni | **7** | | Litakuwa ni jukumu la kila mmiliki au mtunza hoteli/ Nyumba ya kulala wageni kuhakikisha kuwa;<br><br>a. Kuna ulinzi wa kutosha na madhubuti wa wageni na mali zao na kuhakikisha kuwa milango na madirisha ya kila chumba ni imara.<br>b. Kuweka au kutoa mahitaji muhimu kwa wageni katika kila chumba ambayo ni sabuni ya kuogea,mswaki,dawa ya meno,kondom,maji ya moto,taulo, mashuka na mahitaji mengine muhimu kwa wageni.<br>c. Kutoa stakabadhi za kieletroniki kwa kila mgeni mara baada ya kupokea malipo ya chumba kwa kila siku.<br>d. Kuhakikisha anatunza nyaraka /stakabadhi za malipo ya ushuru wa Nyumba za kulala Wageni alizopewa kutoka halmashauri baada ya kulipa ushuru wa kila mwezi.<br>e. Kuhakikisha anaajiri watumishi wa Nyumba za kulala wageni waaminifu na wenye uwezo wa kufuata na kuzingatia masharti ya kusimamia na kuendesha biashara ya Nyumba za Kulala Wageni / |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | hoteli. |
| Kibali cha kuendesha biashara ya Nyumba ya kulala wageni | 8 | | Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni kitatolewa kwa mmiliki baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa katika jengo hilo kuna vitu vifuatavyo;<br>a) Mwanga na hewa ya kutosha;<br>b) Nafasi na samani za kutosha;<br>c) Mfumo wa uondoshaji wa maji taka na taka ngumu wa kuaminika<br>d) Usafi wa jumla wa jengo na vifaa vyake;<br>e) Vyoo na mabafu kwa jinsi zote;<br>f) Vifaa vya zima moto;<br>g) Tenki la kuhifadhia maji safi;<br>h) Vyoo na bafu vilivyosakafiwa vyema kwa vigae au marumaru na kuta zake ziwe zimewekwa vigae kiasu futi sita kutoka usawa wa sakafu;<br>i) Kuwa na jozi Zaidi ya mbili za mashuka, foronya za mito na magodoro kwa kila kitandana na ziwe na rangi isiyoficha uchafu<br>j) Kuwepo na sehemu maalumu ya kufulia na kuanikia nguo;<br>k) Stoo na chumba cha kubadilishia nguo kwa ajili ya wafanyakazi wa hoteli/ nyumba husika ya kulala wageni. |
| Makosa na adhabu | 9 | (1) | Mtu yeyote ambaye;<br>(a)Atakuwa na kitabu cha wageni Zaidi ya kimoja,<br>(b)Atatumia Dafati la wageni |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | lisilotolewa na halmashauri na lisilo na nembo ya halmashauri,<br>(c) Atachana karatasi la Daftari la Wageni kwa lengo la kupunguza na kukwepa kulipa ushuru kamili unaotakiwa kulipwa,<br>(d) Atamruhusu mgeni kuingia katika chumba cha kulala bila kujisajili katika daftari la wageni,<br>(e) Hatoandikisha jina au majina ya wageni waliolala kwenye hoteli/nyumba husika ya kulala wageni;<br>(f) Atamruhusu mgeni kuingia chumbani bila kujaza daftari la wageni kikamilifu,<br>(g) Atamzuia Afisa Mwidhiniwa kufanya ukaguzi katika nyumba ya kulala wageni au hoteli;<br>(h) Atakiuka kipengele chochote cha sheria ndogo hizi.<br>(i) Atamshawishi mtu mwingine asilipe ushuru,<br>(j) Atatumia mbinu yoyote kwa lengo la kukwepa kulipa ushuru unaostahili kulipwa,<br>(k) Atatoa takwimu za uongo juu ya wageni waliolala katika hoteli/ nyumba ya kulala wageni kwa lengo la kukwepa kulipa ushuru sahihi, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | (l) Atakataa kukaguliwa kwa kuwazuia wakaguzi kuingia katika hoteli / nyumba ya kulala wageni,<br>(m)Atatoa lugha ya kashfa au kejeli kwa Afisa muidhiniwa au timu ya ukaguzi ya wataalam katika utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br>(n)Atakataa kulipa ushuru kwa makusudi,<br>(o)Atashindwa kufuata masharti ya uendeshaji wa nyumba za kulala wageni ipasavyo, |
| | | (2) | Mtu huyo atakuwa amekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi, na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi za kitanzania milioni moja 1,000,000/= au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote kwa pamoja yaani kifungo na faini. |
| oKufifilisha kosa | 10 | | Iwapo mtu aliyetenda kosa chini ya Sheria hizi atakiri makosa kabla shauri halikufikishwa mahakamani na kulipa faini kwa hiari, Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa lake baada ya mkosaji kujaza fomu kwa Mujibu wa Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi. |

## JEDWALI LA KWANZA

## HATI YA KUKIRI KUTENDA KOSA

**(Chini ya Kifungu 10)**

Mimi ………………………………………………………….…………………. Nakiri mbele ya Bw/Bi ………………………………………………….. Mkurugenziwa Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwambaMnamo tarehe....................... Ya Mwezi ………………………… mwaka ………………………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu namba ……………………………….. Cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Nyumba za Kulala za Wageni) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka, 2024.

Nipo tayari kulipa kiasi cha faini kinachodaiwa ambacho ni Tshs. ______________________ badala ya kupelekwa Mahakamani, ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo hizi. Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu huku nikifahamu kuwa nilichofanya ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo za (Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka 2024.

Jina la Mkosaji:_____________________________________Saini________________________

Alama ya dole gumba _________________________Tarehe _____________saa_______

**Mbele ya Ushahidi wa.**

Jina:_____________________________________________Saini_____________________ ____ Alama ya dole gumba ______________________________ Tarehe_______________________

Maelezo ya Mkurugenzi _______________________________________________________

Jina laMkurugenzi: ____________Saini ya Mkurugenzi: ______Tarehe _________

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea iligongwa katikaSheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutanowa Baraza la Madiwani wa Halmashauri yaManispaa ya Songea uliofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri tarehe …………. Mwezi …………, 2024 na Lakiri hii iligongwa mbele ya:

________________________________

BASHIR P. MUHOJA,

**MKURUGENZIHALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA.**

________________________________

MICHAEL LEODGAR MBANO

**MSTAHIKI MEYA HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA.**

NAKUBALI

________________________________

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)

**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS,**

**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)**

**DODOMA**

TAREHE _________

**SHERIA YA SERIKALI ZAMITAA (MAMLAKA ZA MIJI)**

**SURA YA 288/2002.**

**SHERIA NDOGO.**

## Zimetungwa chini ya kifungu cha 89 (1).

**SHERIA NDOGO ZA (KUDHIBITI UBORA WA VYAKULA NA MAJENGO YAVYAKULA)ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA, 2024.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jina la tarehe ya kuanza kutumika | **1.** | | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (**Kudhibiti Ubora wa Vyakula na Majengo yaVyakula)** za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka, 2024 na zitaanza kutumika mara baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali. |
| Eneo la kutumika | **2.** | | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea. |
| **Tafsiri** | **3.** | | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:- |
| | | | **"Afisa Muidhiniwa"** Maana yake Afisa Afya yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>'**Afya'**maana yake ni ukamilifu wa mwili kiakili, na kijamii.<br><br>**"Halmashauri"** Maana yake Halmashauri ya Manispaa ya Songea;<br><br>**"Chakula"** Maana yake ni kitu chochote kinacholiwa na binadamu isipokuwa dawa.<br><br>**'Chakula safi"** maana yake ni chakula kilichohifadhiwa,andaliwa, na kuliwa katika eneo ambalo halina uchafu au chakula kisichochafuliwa na uchafu. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ‘**Chakula salama’** maana yake ni chakula ambacho hakina vimelea vya magonjwa.<br><br>‘**Majengo ya Vyakula**’ maana yake ni majengo yoyote yaliyojengwa katika Halmashauri na kuidhinishwa na halmashauri yatumike kwa kuhifadhia, kuandalia, kupikia, kulia vyakula na kuuzia vyakula.<br><br>**“Mfanyabiashara wa Chakula”**maana yake ni mtu yeyote anayejihusisha na biashara ya kuandaa, kuhifadhi na kuuza kitu chochote kinacholiwa na binadamu isipokuwa dawa.<br><br>**“Mkurugenzi”** Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea ikiwa ni pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya MkurugenzI.<br><br>‘**Uchafu’** maana yake ni kitu chochote ambacho kipo mahali pasipo stahili kuwepo. |
| Mamlaka ya udhibiti | 4 | | Halmashauri inaanzisha utaratibu maalum wa kudhibitibiashara ya vyakula na Majengo ya kuuzia vyakula ndani ya Halmashauri. |
| Usajili wa biashara | 5. | (1) | Ni wajibu wa kila Mfanyabiashara ndani ya Halmashauri kufanya yafuatayo; |
| | | | a. Kutoa taarifa ya kujenga jengo la biashara ya chakula kwa Mkurugenzi kabla ya kuanza shughuli za ujenzi kwa kujaza fomu ya maombi kwa mujibu wa Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.<br>b. Kuchora ramani ya jengo la chakula kwa kufuata mtiririko ulioelezwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | katika kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hizi na kupeleka kwa Mkurugenzi kwa ajili ya kuihakiki kulingana na Sheria za Mipango Miji namba 8 za Mwaka 2007 |
| | | (2) | Baada ya Wataalam kuihakiki ramani na kuona inafaa, mwombaji atapewa kibali cha ujenzi kwa ajili ya ujenzi husika. |
| | | (3) | Mfanyabiashara atatakiwa kutoa taarifa ya kukamilika kwa ujenzi wa jengo husika kwa Mkurugenzimara moja ili Afisa Muidhiniwa aende kukagua jengo hilo baada ya mfanyabiashara kulipa ada ya ukaguzi wa jengo husika ya shilingi hamsini Elfu ( Tshs; 50,000/=) |
| | | (4) | Afisa Muidhiniwa akithibitisha kuwa jengo hilo limekidhi viwango na ubora kama ilivyotajwa katika kifungu cha 6cha Sheria Ndogo hizi, atamruhusu Mfanyabiashara ajaze fomuya maombi ya biashara ya chakula kwa Mujibu wa Jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi. |
| Usafi wa chakula | **6.** | | Kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi,ili kuhakikisha usafi wa Chakula unazingatiwa, sharti jengo la Chakula liwe na sifa zifuatazo;<br>a. Sakafu iliyotengenezwa kwa zege na kumaliziwa kwa saruji au marumaru,<br>b. Kuta zilizojengwa imara kwa tofari za kuchomwa, au zilizotengenezwa kwa saruji na kupigwa lipu ya kuchanganywa kwa mchanga na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | saruji na kupakwa rangi, na urefu wa ukuta usipungue mita tatu,<br>c. Dari iwe imara iliyotengenezwa kwa mbao, au gypsum au chipboard na kupakwa rangi,<br>d. Paa liwe limepauliwa kwa boriti za miti au vyuma na kuezekwa kwa bati, au vigae au zege,<br>e. Milango iwe na upana usiopungua sentimeta tisini na iwe na kifuniko cha mbao au aluminium,<br>f. Dirisha liwe ni sehemu ya moja ya nane ya kuta katika Chumba, pia liwe na kifuniko cha kioo au Aluminium. |
| Wajibu wa Mfanyabiashara wa Chakula | **7.** | (1) | Kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kila Mfanyabiashara wa Chakula anatakiwa kuhakikisha jengo lake linakuwa na vyumba vifuatavyo;<br>I. Stoo,<br>II. Chumba cha kuandalia Chakula,<br>III. Jiko,<br>IV. Chumba cha kupakulia chakula,<br>V. Chumba cha kulia Chakula,<br>VI. Chumba cha kuoshea vyombo ,<br>VII. Chumba cha kubadilishia nguo watumishi wake.<br>VIII. Katika vyumba vyote vilivyotajwa kuanzia namba (i) hadi (vii) hapo juu, kila chumba kinatakiwa kuwa na sinki la kunawia mikono. |
| | | (2) | Ni wajibu wa Mfanyabiashara wa chakula kuwa na Choo bora kwenye jengo lake la biashara chenye sifa zifuatazo;<br>I. Choo kinachotumia Maji (Water |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Closet pan)<br>II. Sehemu ya kunawia mikono ( Wash hand basin) yenye sabuni ya maji na koki ya kufunga kwa kiwiko cha mkono;<br>III. Kuwe na kabati safi la aluminium la kuhifadhia vyombo lenye vioo ambalo linasafishika na lisilo ruhusu wadudu na vumbi kuingia.<br>IV. Awe na vyombo vya kuhifadhia taka taka, kimoja kiwekwe eneo la nje ya jengo na chombo cha kuhifadhia mabaki ya chakula kiwekwe eneo la ndani ya jengo la chakula.<br>V. Kusafisha maeneo yanayozunguka jengo la chakula ili kuondoa mazalio ya wadudu na wanyama wanaoeneza magonjwa kwa njia ya chakula. |
| | | 3 | Bila kuathiri masharti yaliyoelezwa katika kifungu cha 7 (2) hapo juu, kwa maeneo yote ambayo hayana mtandao wa Maji ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Songea (SOUWASA), mfanyabiashara wa chakula anatakiwa kuwa na choo imara chenye shimo lisilopungua futi nane (8), paa imara, milango, na mfuniko wa tundu kwa ajili ya kuzuia wadudu kutoka na pia kuhakikisha choo hicho kinatumika wakati wote na kiwe na maji tiririka. |
| | | 4 | Ni wajibu wa kila mfanyabiashara wa Chakula kuhakikisha yafuatayo;<br>I. Watumishi wake wote wamepimwa afya, angalau mara moja ndani ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kipindi chamiezi sita (6) na Mganga Mkuu wa Halmashauri (Municipal Medical Officer of Health).<br>II. Watumishi wote wanavaa sare maalum za kazi wawapo kazini;<br>a. Kofia nyeupe,<br>b. Viatu vya kutumbukiza au kwa watumishi wa duka la nyama na sehemu ya kuoka mikate lazima wavae buti nyeupe (gum boot),<br>c. Koti jeupe. |
| Wajibu wa halmashauri na Afisa Muidhiniwa | 8 | (1) | Utakuwa ni wajibu wa Halmashauri kuhakikisha inapima kupitia maabara maalum chakula chochote kitakachokamatwa na kuhisiwa kuwa sio chakula salama kabla ya kutoa faini kwa mfanyabiashara wa chakula hicho. |
| | | (2) | Halmashauri inao wajibu wa kisheria katika Sheria Ndogo hizi, kuhakikisha inatimiza wajibu wake ndani ya siku saba (7) za kazi mara inapopata maombi ya kufanya ukaguzi wa jengo la chakula. |
| | | (3) | Ni wajibu wa Afisa Muidhiniwa kuingia na kufanya ukaguzi katika jengo la Chakula katika siku na saa za kazi bila kuzuiwa na mtu yeyote. |
| | | (4) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi,Afisa Muidhiniwa anao wajibu wa kisheria kutenda haki kwa kila mtu bila kufanya upendeleo na uonevu wakati wa  ukaguzi wa majengo ya vyakula. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | (4) | Afisa Muidhiniwa ana wajibu kutoa stakabadhi ya kieletroniki (EFD) kwa malipo yote yatokanayo na ada na faini zitokanazo na Sheria Ndogo hizi. |
| Makosa na adhabu | 9 | (1) | Mtu yeyote ambaye:-<br>a) Atajenga jengo la chakula bila idhini ya Halmashauri<br>b) Atakuwa na jengo la chakula ambalo halina ubora,<br>c) Atakuwa na choo kibovu,<br>d) Atakuwa hana choo,<br>e) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukiuka matakwa ya Sheria Ndogo hizi,<br>f) Atakataa kuuza, kuhifadhi, kusambaza au kutupa vyakula vilivyoisha muda wa matumizi,<br>g) Atakataa au kushindwa kutii maagizo ya Afisa Muidhiniwa ,<br>h) Atamzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake,<br>i) Atatishia uhai wa Afisa Muidhiniwa wakati akitekeleza majukumu yake,<br>j) Atamzuia Afisa Muidhiniwa kuingia katika jengo la chakula kufanya ukaguzi,<br>k) Atashindwa kutii matakwa ya Sheria Ndogo hizi kwa namna yoyote. |
| | | (2) | Mtu huyoatakuwa amekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi, akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki moja tu (**Tshs;100,000/=)** au kifungo cha miezi isiyozidi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja, kifungo na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | faini. |
| | | (3) | Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 9 (2) cha Sheria Ndogo hizi, endapo katika ukaguzi wa jengo la chakula itagundulika mfanya biashara amekiuka Sheria Ndogo hizi, Afisa muidhiniwa atampa mfanyabiashara huyo notisi ya kufunga mara moja biashara wakati akisubiri kufanya marekebisho ya mapungufu yaliyopatikana baada ya kulipa faini. |
| | | (4) | Endapo mfanyabiashara wa chakula amefungiwa biashara, kuharibiwa vyakula au kutupwa kwa vyakula visivyo salama kwa mlaji au kuamuriwa kufanya marekebisho katika jengo lake la chakula, hatafunguliwa biashara yake hata kama amelipa faini aliyostahili kulipa hadi atakapokamilisha marekebisho aliyoamuriwa ayafanye kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi. |
| | | (5) | Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea kwa mfanyabiashara wa chakula kwa kufungiwa kwa biashara yake, kuharibiwa au kutupwa kwa vyakula vyake kutokana na mapungufu yaliyopatikana katika biashara yake, kwa kutekeleza mamlaka yakekwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi. |
| Kufifilisha kosa | **10.** | | Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote yule endapo mkosaji, atakiri kosa lake kwa maandishi kwa kujaza fomu kwa mujibu wa jedwali la tatu la Sheria Ndogo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | hizi na kukubali kulipa faini. |

**JEDWALI LA KWANZA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

**(NEMBO YA HALMASHAURI)**

**FOMU YA UTOAJI WA TAARIFA ZA UJENZI WA JENGO LA CHAKULA**
**(Chini ya kifungu cha 5 (1) (a)).**

Jina la Mtoaji wa Taarifa…………………………………………………………………..

Namba ya kiwanja……………………………Kitalu……………………………………….

Mtaa……………………………Kata……………………Namba ya simu …………………

Hali ya ukamilifu wa Jengo (A ) 100%,( B) 75%..........................

Mimi …………………………………………..Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli kuwa Jengo langu limekamilika kwa asilimia …………………...

**Naomba Wataalam wa Afya waje walikague**.

Jina…………………………………………………

Sahihi……………………………………………..

Tarehe…………………………………………….

JEDWALI LA PILI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA

(NEMBO YA HALMASHAURI)

FOMU YA MAOMBI YA BIASHARA YA CHAKULA

(Chini ya kifungu cha 5(4) ).

MKURUGENZI WA MANISPAA

SLP 14

SONGEA

## SEHEMU YA KWANZA; MAELEZO YA MWOMBAJI.

Mimi/Sisi…………………tunaomba kibali / kuhuwisha kibali cha kutengeneza, kuuza, kusindika,kuhifadhi au kusambaza vyakula vifuatavyo …………

1. Jina la Mwombaji…………………………………………………………………..
2. Anuani……………………………………….simu…………………………………
3. Mahali jengo lilipo; Mtaa……………..Kata…………………………………….
4. Namba ya Usajili wa Jengo…………………..Mwaka…………………………
5. Namba ya Kibali cha Zamani..................Chtarehe…………Mwaka………………
6. Tarehe……..Saini ya Mwombaji………………Alama ya Dole gumba.

## SEHEMU YA PILI;KWA MATUMIZI YA OFISI.

1. Kibali na………………………………………………………….
2. Kimethibitishwa na …………………………………………………..
3. Tarehe……………………….Saini…………………………Au Dole gumba.

JEDWALI LA TATU

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA

(NEMBO YA HALMASHAURI)

**HATI YA KUKIRI KWA HIARI KUTENDA KOSA.**

**(Chini ya kifungu cha 10).**

Mimi:________________________nakiri mbele ya Bw/Bi:_____________Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwamba mnamo tarehe:______________ya mwezi________mwaka__________nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu namba_________________cha Sheria Ndogo za **(KudhibitiUbora wa vyakula na Majengo ya vyakula**) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka 2024.

Nipo tayari kulipa kiasi cha faini kinachodaiwa ambacho ni Tshs______________badala ya kupelekwa Mahakamani ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopo chini ya kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwahiari yangu kadri ya ufahamu wangu huku nikifahamu kuwa nilichofanya ni kosa kwa Mujibu wa Sheria Ndogo za **(Kudhibiti Ubora wa vyakula na Majengo ya Vyakula)** za Halmashauri ya Manispaa ya Songea, za mwaka 2024.

Jina la Mkosaji:__________saini____________alama ya dole gumba ____tarehe_______

**Mbele ya Shahidi:**

Jina:_________Saini___________Alama ya dole gumba__________tarehe:__________

Maelezo ya Mkurugenzi kwa kifupi:- ________________________________

Jina la Mkurugenzi:____________________________________________________

Saini ya Mkurugenzi:_______________________________________________________

Tarehe:__________________________________________________________________

Mhuri:________________________________________________________________

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea iligongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea uliofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri tarehe _______ mwezi _________ 2024 na Lakiri hii iligongwa mbele ya:

___________________________________

BASHIR P. MUHOJA,

**MKURUGENZIHALMASHAURI YAMANISPAA**

**SONGEA**

___________________________________

MICHAEL LEODGAR MBANO,

**MSTAHIKI MEYA HALMASHAURI YAMANISPAA**

**SONGEA**

NAKUBALI

___________________________________

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)

**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS,**

**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)**

**DODOMA**

TAREHE ______/_______/_________

**SHERIA YA SERIKALI ZAMITAA (MAMLAKA ZA MIJI)**

**SURA YA 288/2002.**

**SHERIA NDOGO.**

**Zimetungwa chini ya kifungu cha 89.**

**SHERIA NDOGO ZA (KUDHIBITI UTIRIRISHAJI WA MAJITAKA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2024**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jina la tarehe ya kuanza kutumika** | **1.** | | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Kudhibiti Utiririshaji wa Majitaka) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka, 2024 na zitaanza kutumika mara baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali. |
| **Eneo la kutumika** | **2.** | | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea. |
| **Tafsiri** | **3.** | | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:- |
| | | | **"Afisa Muidhiniwa"** Maana yake Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>**"EWURA'** maana yake ni Mamlaka ya udhibiti wa huduma za Nishati na Maji Tanzania.<br><br>**"Halmashauri"** Maana yake Halmashauri ya Manispaa ya songea.<br><br>"**Majitaka"**maana yake ni maji machafu baada ya matumizi kutoka kwenye makaro ya kuoshea vyombo, uchafu na maji toka vyooni na kwenye mabafu.<br><br>**"Mkurugenzi"** Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea na ni pamoja na Afisayeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.<br><br>"**Mmiliki wa nyumba**" maana yake mtu yeyote anayemiliki jengo lolote ndani ya Halmashauri.<br><br>**"SOUWASA"** maana yake Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Songea Mjini.<br><br>**"Wakala"** Ina maana ya mtu binafsi, kikundi cha watu, Kampuni, Taasisi, Shirika au Serikali ya Mtaa atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi. |
| **Uanzishaji wa utaratibu maalum wa udhibiti wa** | **4.** | (1) | Halmashauri imeanzisha utaratibu maalumu wa kudhibiti utiririshaji wa Majitaka ndani ya mamlaka |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Maji taka** | | | ya Halmashauri. |
| | | (2) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kila mmiliki wa nyumba ndani ya Halmashauri anatakiwa kuunganisha mifumo ya maji taka ya nyumba yake na Mfumo wa Majitaka wa SOUWASA. |
| **Wajibu wa Mmiliki wa nyumba** | **5.** | (1) | Utakuwa ni wajibu wakila Mmiliki wa nyumba ndani ya eneo la mamlaka ya Halmashauri kuhakikisha jengo lake limeunganishwa na Mfumo wa Majitaka wa SOUWASA kwa maeneo yote ambayo mifumo ya majitaka ya SOUWASA imeshajengwa na kuanza kutumika. |
| | | (2) | Ni kosa kwa Mmiliki yeyote wa nyumba ndani ya mamlaka ya Halmashauri kushindwa kuunganisha mfumo wa Majitaka wa nyumba yake na mfumo wa Majitaka wa SOUWASA kinyume na utaratibu ulioelezwa katika kifungu cha 5(1); |
| **Wajibu wa Halmashaurii** | 6 | (1) | Kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi,halmashauri itakuwa na wajibu wa kuhakikisha ramani zote za majengo zitakazokuwa zinapitishwa kwa ajili ya kutoa vibali vya ujenzi zinazingatia uwepo wa mifumo ya majitaka iliyoelekezwa katika miundombinu ya SOUWASA. |
| | | (2) | Halmashauri inaweza kukataa kupitisha ramani yoyote ya jengo ambayo haijazingatia masharti yaliyoelekezwa katika kifungu cha 6(1) hapo juu. |
| **Wajibu wa SOUWASA** | **7.** | (1) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, SOUWASA ina wajibu wa kuhakikisha maeneo yote ya Halmashauri yanafikiwa na mfumo wa Majitaka ili kurahisisha wamiliki wa nyumba kuunganisha mifumo ya Majitaka ya nyumba zao. |
| | | (2) | Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 7(1) cha Sheria Ndogo hizi,SOUWASA itatoa huduma ya kuondoa majitaka kwa viwango maalum vya malipo vilivyoidhinishwa na EWURAkwa kutumia magari maalum ya kunyonya majitaka kwa maeneo yote ambayo mifumo ya majitaka ya SOUWASA haijajengwa. |
| **Gharama za kuunganisha mifumo y a maji taka** | **8.** | | Kila Mmiliki wa nyumba atalazimika kulipia gharama za kuunganishiwa mfumo wa Majitaka katika nyumba yake kulingana na viwango vya SOUWASA. |
| **Wajibu wa kulipa gharama kabla ya huduma** | **9.** | (1) | Utakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba ndani ya Halmashauri kulipia gharama za kuunganishiwa mfumo wa Majitaka katika nyumba |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | yake kabla ya kupata huduma toka SOUWASA. |
| | | (2) | Gharama zinazolipwa SOUWASA zitakuwa kwa ajili ya ununuzi wa Vifaa na vibarua ili kufanikisha zoezi la kuunganisha nyumba ya mmiliki na mfumo wa Majitaka wa SOUWASA. |
| **Wajibu wa Serikali ya Mtaa** | **10.** | (1) | Utakuwa ni wajibu wa kila Serikali za Mitaa ndani ya mamlaka ya Halmashauri kuhakikisha kila Mmiliki wa nyumba katika Mtaa husika ameunganishwa naMfumo wa Majitaka wa SOUWASA; |
| | | (2) | Serikali za Mitaazinaweza kufuatilia na kujiridhisha endapo mmiliki wa nyumbaanazingatiamatakwa ya Sheria Ndogo hizi. |
| **Uteuzi wa Wakala /Afisa muidhiniwa** | **11.** | (1) | Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Halmashauri inaweza kumteua Wakala au Afisa muidhiniwa kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi; |
| | | (2) | Wakala au Afisa muidhiniwa atakayeteuliwa na Halmashauri atakuwa na jukumu la kuhakikisha matakwa ya Sheria Ndogo hizi yanatekelezwa na kutoza faini kwa niaba ya Halmashauri kama ilivyoelezwa na Sheria Ndogo hizi; |
| **Makosa na adhabu** | **12.** | (1) | Mtu yeyote ambaye:-<br>a) Atakataa kuunganisha nyumba yake na mfumo wa Majitaka kinyume na Sheria Ndogo hizi,<br>b) Atakataa kulipia gharama za kuunganisha mfumo wa majitaka kama zilivyotolewa na SOUWASA<br>c) Atakwepa kwa makusudi kuunganisha mfumo wa Majitaka wa SOUWASA katika nyumba yake,<br>d) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukiuka matakwa ya Sheria Ndogo hizi,<br>e) Atakataa au kushindwa kutii maagizo ya Afisa Muidhiniwa au Wakala,<br>f) Atamzuia Afisa Muidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake,<br>g) Atatishia uhai wa wakala au Afisa Muidhiniwa wakati akitekeleza majukumu yake,<br>h) Atatoa maneno ya kupotosha jamii juu ya matakwa ya Sheria Ndogo hizi,<br>i) Akajichukulia uamuzi kutangaza hadharani kuwazuia watu wengine wasitekeleze matakwa ya Sheria Ndogo hizi. |
| | | (2) | Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na atashtakiwa mahakamani akipatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi mia tano elfu tu ((**Tshs;500,000/=)** au kifungo cha miezi isiyozidi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja; |
| **Kufifilisha kosa** | **13.** | | Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote yule endapo mkosaji, atakiri kosa lake kwa maandishi kwa kujaza fomu kwa mujibu wa jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini. |

## JEDWALI LA KWANZA

## HATI YA KUKIRI KUTENDA KOSA

**(Chini ya Kifungu 13)**

Mimi …………………………Nakiri mbele ya Bw/Bi ……………………………… Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwamba Mnamo tarehe...................... ya Mwezi ………………………… mwaka ………………………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu namba ……………………………….. Cha Sheria Ndogo za (Kudhibiti Utiririshaji wa Majitaka) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka, 2024.

Nipo tayari kulipa kiasi cha faini kinachodaiwa ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 13 cha Sheria Ndogo hizo.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Jina: ……………………………………….. Saini ………………………………………………

Alama ya dole gumba …………………………………Tarehe ………………………………

**Mbele ya Ushahidi wa.**

Jina: …………………………………………. Saini ……………………………. Alama ya dole gumba …………………………………….. Tarehe …………………………….

Maelezo Mafupi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa………… ……………

Jina laMkurugenzi …………………………… Saini ………………… Tarehe ……………….

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea iligongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio laMkutano wa Baraza la Madiwani ulioketi Ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songeatarehe ________________mwezi____________mwaka, 2024, na kushuhudiwa na:-

_____________________________________

BASHIR P. MUHOJA,

**MKURUGENZI HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA.**

_____________________________________

MICHAEL LEODGAR MBANO,

**MSTAHIKI MEYA HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA.**

**NAKUBALI;**

______________________

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (**MB),**

**WR-OR TAMISEMI.**

**DODOMA**

**Tarehe:___________________**

**Tangazo la Serikali Na…………..La Tarehe………………..**

**SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)**

**SURA YA 288**

**Zimetungwa chini ya kifungu cha 89**

**SHERIA NDOGO ZA USAFI WA MAZINGIRA(MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA, 2024.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jina la Sheria Ndogo na tarehe ya kuanza kutumika | **1.** | | Sheria hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Usafi wa mazingira (Marekebisho) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka, 2024 na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Songea za mwaka, 2014 GN. 308 la tarehe 31 Julai, 2015 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. |
| Marekebisho GN. 308 ya tarehe 31 Julai, 2015 | **2** | | Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 3 kwa kutafsiri maneno yafuatayo;<br>"Halmashauri" maana yake halmashauri ya Manispaa ya Songea.<br>"Soko" maana yake ni eneo lililotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya huduma za kuuza na kununua bidhaa.<br>' Taasisi binafsi' maana yake Taasisi zote zisizo za serikali. |
| Marekebisho GN. 308 ya tarehe 31 Julai, 2015 | **3.** | | Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 6(2) kwa kuongeza kifungu cha 6 (2) (a) na kusomeka 'itakuwa ni wajibu wa kila kaya, mfanyabiashara, taasisi na ofisi binafsi kutoa ada ya uzoaji taka kila mwezi kulingana na viwango vilivyowekwa vya ada ya uzoaji taka katika jedwali la Sheria Ndogo hizi'. |
| Marekebisho GN 308 ya tarehe 31 Julai, 2015. | **4** | | Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho kwa kufuta kifungu cha 24, 32 (1), (2) na 34 |
| Marekebisho GN 308 ya tarehe 31 Julai, 2015 | **5** | | Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 33 kwa kukiandika upya na kusomeka "Kila mfanyabiashara katika maeneo mbalimbali ya halmashauri atawajibika kulipa ada ya uzoaji taka kama inavyooneshwa katika jedwali A |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Marekebisho GN 308 ya tarehe 31 Julai, 2015 | **6** | | Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 35 kwa kuandika upya kifungu chote na kusomeka ‘ Kila mtumishi anayefanya kazi katika mgahawa, hotel, bar, grocery ,nyumba za kulala wageni na viwandani analazimika kupima afya yake katika kipindi cha kila miezi sita (6) kwa kulipa ada ya upimaji afya ya Tshs 5000 /= |
| Marekebisho GN. 308 ya tarehe 31 Julai, 2015 | **7.** | | Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 36 eneo la makosa kwa kuongeza;<br>a) Kifungu cha 36 (k) kuwa atakataa kulipa ada ya uzoaji taka kulingana na viwango vilivyowekwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.<br>b) Kifungu cha 36 (l) atamshawishi mtu mwingine asilipe ada ya uzoaji taka.<br>c) Kifungu cha 36 (m) atatupa taka ovyo katika maeneo yasiyo ruhusiwa.<br>d) Kifungu cha 36 (n) atamwaga taka barabarani kutokana na bidhaa anazosafirisha kama vile makaa ya mawe, mchanga, udongo, mawe, kifusi, nafaka na kadharika.<br>e) Kifungu cha 36 (o) atatiririsha maji machafu kutoka kwenye nyumba anayoishi, ofisi, eneo lake la biashara nk<br>f) Kifungu cha 36 (p) ataanzisha gereji ya kutengeneza magari na kupaka rangi magari katika maeneo yasiyoruhusiwa au kwenye nyumba za makazi.<br>g) Kifungu cha 36 (q) ataweka /atatupa taka katika maeneo ya mbele ya nyumba yake ya kuishi, nyumba ya biashara, ofisi, soko au pembezoni mwa barabara.<br>h) Kifungu cha 36 (r) atashindwa kufanya usafi katika eneo lake la biashara au nyumba yake ya makazi.<br>i) Kifungu cha 36 (s) atashindwa kupima afya yake katika kipindi cha kila miezi sita (6). |
| Marekebisho GN. 308 ya tarehe 31 Julai, 2015 | **8** | | Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika jedwali la kwanza la ada ya uzoaji taka na kusomeka kwa mujibu wa jedwali A na B la marekebisho haya. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Marekebisho GN 308 ya tarehe 31 Julai, 2015 | **9** | | Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika eneo la adhabu katika kifungu cha 36 na badala yake kuweka maneno yanayosomeka “Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na endapo atapatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (Tshs 200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (Tshs1,000,000/=) au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili kwa pamoja. |

JEDWALI ‘A

ADA ZA USHURU WA TAKA

| Na | AINA YA BIASHARA / KAYA | KIWANGO KWA MWEZI | KIWANGO KWA MWAKA |
|---|---|---|---|
| 1 | Kaya | 2,000/= | 24,000/= |
| 3 | Duka la rejareja | 4,000/= | 48,000/= |
| 4 | Duka la jumla | 10,000/= | 120,000/= |
| 5 | viwanda vya kuchakata nafaka | 7000/= | 84,000/= |
| 6 | Viwanda vya Uselemala | 5,000/= | 60,000/= |
| 7 | Mashine za mbao | 5,000/= | 60,000/= |
| 8 | Hotel | 30,000/= | 360,000/= |
| 9 | Mgahawa | 30,000/= | 360,000/= |
| 10 | Mama / baba lishe | 3,000/= | 36,000/= |
| 11 | Grocery / vilabu vya pombe | 5,000/= | 60,000/= |
| 12 | Bar kubwa/ kumbi za starehe | 80,000/= | 960,000/= |
| 13 | Gereji | 10,000/= | 120,000/= |
| 14 | Nyumba za kulala wageni | 5,000/= | 60,000/= |
| 15 | Nyumba za sinema | 7,000/= | 84,000/= |
| 16 | Saloon ya kike na kiume/ massage | 5,000/= | 60,000/= |
| 17 | Kituo cha Mafuta (Petrol station) | 30,000/= | 30,000/= |
| 18 | Ghala (Godown) | 7,000/= | 84,000/= |
| 19 | Biashara ya chips | 25,000/= | 300,000/= |
| 20 | Bucha za nyama / samaki | 4,000/= | 48,000/= |
| 21 | Mafundi kushona nguo | 5,000/= | 60,000/= |
| 22 | Mafundi vyuma (wahunzi) | 5,000/= | 60,000/= |
| 23 | Majengo ya kuoshea magari/pikipiki | 5,000/= | 60,000/= |
| 24 | Stoo za mkaa | 5,000/= | 60,000/= |
| 25 | Biashara ya matunda / miwa | 2,000/= | 24,000/= |
| 26 | Biashara ya kuuza Mbogamboga | 2,000/= | 24,000/= |
| 27 | Vizimba / meza za sokoni | 2,000/= | 24,000/= |
| 28 | Biashara ya urembo | 2,000/= | 24,000/= |
| 29 | Biashara ya shoe shine | 2,000/= | 24,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 29 | Biashara ya nguo/viatu vya mitumba | 3,000/= | 36,000/= |
| 30 | Mfanyabiashara minadani | 2000/= | 24,000/= |

JEDWALI ‘B’

ADA YA UZOAJI TAKA KATIKA MAJENGO YA TAASISI KAMPUNI/ OFISI BINAFSI

| **Na** | **AINA YA TAASISI/OFISI** | **KIWANGO KWA MWEZI** | **KIWANGO KWA MWAKA** |
|---|---|---|---|
| 1. | Benki ( NMB, CRDB, TCB, NBC,AZANIA nk) | 50,000/= | 600,000/= |
| 2. | Taasisi zote za Umma ( TRA, TTCL, POSTA,BIMA , NSSF nk) | 50,000/= | 600,000/= |
| 3. | Taasisi binafsi | 10,000/= | 120,000/= |
| 4 | Taasisi za kidini | 10,000/= | 120,000/= |
| 5 | Kiwanda kidogo | 100,000/= | 1,200,000/= |
| 6 | Kiwanda cha kati | 200,000/= | 1,800,000/= |
| 7 | Kiwanda kikubwa | 300,000/= | 2,400,000/= |
| 8 | Ofisi binafsi | 10,000/= | 120,000/= |
| 9 | Kampuni za mabasi | 30,000/= | 360,000/= |
| 10 | Taasisi nyingine za kifedha | 10,000/= | 120,000/= |
| 11 | Kampuni nyinginezo | 10,000/= | 120,000/= |
| 12 | Vituo binafsi vya huduma za afya | 10,000/= | 120,000/= |
| 13 | Shule/vyuo binafsi | 20,000/= | 240,000/= |

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea iligongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea uliofanyika katika ukumbi wa Halmashauri tarehe ……….. Mwezi …….. Mwaka 2024 Mhuri huo umegongwa mbele ya :-

BASHIR P. MUHOJA,

**MKURUGENZI HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA.**

MICHAEL LEODGAR MBANO

**MSTAHIKI MEYA HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA.**

**NAKUBALI;**

MOHAMED OMARY MCHENGERWA **(Mb),**

**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS,**

**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.)**

**DODOMA,**

**Tarehe: ___________________**